

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Thelathini na Tisa – Tarehe 5 Juni, 2020

(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae, Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA – MAKAMU MWENYEKITI WA
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Nane na Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge.

SPIKA: Ahsante sana Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Ngeleja. Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

(Maswali yafuatayo yameulizwa na kujibiwa kwa njia ya mtandao)

Na. 366

Kuajiri Watendaji wa Vijiji – Vijiji vyote vya Jimbo la Igunga

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU aliuliza:-

Jimbo la Igunga lenye vijiji 68 linao Watendaji wa Vijiji 15 tu walioajiriwa, hali hii inaathiri sana utendaji kazi na usimamizi wa maendeleo katika vijiji hivyo:-

Je, ni lini Serikali itaajiri Watendaji wa Vijiji vyote vya Jimbo la Igunga?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mbunge wa Igunga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Igunga lina vijiji 63 na Watendaji wa Vijiji 24 walioajiriwa. Hivyo, kuna upungufu wa Watendaji wa Vijiji 39. Kwa kutambua changamoto hiyo, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali imetenga nafasi za ajira mpya za Watendaji wa Vijiji 39 kwa ajili ya Halmashauri ya Wilaya ya Igunga ili kuondoa kabisa upungufu huo.

Na. 367

Hitaji la Hospitali ya Wilaya ya Geita

MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA aliuliza:-

Sera ya Taifa inataka kila kijiji kiwe na zahanati, kila kata iwe na kituo cha afya na kila Wilaya iwe na Hospitali:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa inapatikana Hospitali ya Wilaya ya Geita?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lolosia Jeremia Bukwimba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na ujenzi wa hospitali mbili za Halmashauri katika Wilaya ya Geita zinazogharimu jumla ya shilingi bilioni 3.0 kwa pamoja. Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Geita ilipokea fedha shilingi bilioni 1.5 katika mwaka wa fedha 2018/2019 na Hospitali ya Wilaya ya Katoro ilipokea shilingi bilioni 1.5 katika mwaka wa fedha 2019/20 na ujenzi unaendelea.

Na. 368

Hitaji la wataalam wa upimaji ardhi-Tarime

MHE. ESTHER N. MATIKO aliuliza:-

Ili ardhi iwe na thamani lazima ipimwe ili kupelekea wafanyabiashara na wakulima kupata mikopo katika taasisi za fedha na kujiingizia kipato pamoja na Taifa kwa ujumla. Ndani ya Jimbo la Tarime Mjini Kata mbili tu za Bomani na Sabasaba ndizo zimepimwa ardhi kwa 75% kati ya kata nane za Halmashauri ya Mji wa Tarime na hii ni kutokana na upungufu mkubwa wa wataalam wa kupima ardhi.

Je, ni lini Serikali itapeleka wataalam wa kutosha katika Halmashauri ya Mji wa Tarime ili kuweza kupima ardhi kwa Kata zote sita zilizosalia ili wananchi hao waweze kunufaika na ardhi yao?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha utendaji kazi, watumishi wa sekta ya ardhi waliokuwa chini ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI wamehamishiwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Aidha, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeanzisha Ofisi za Ardhi katika Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara kutoka Kanda tisa (9) zilizokuwepo ili kusogeza huduma za sekta karibu zaidi na wananchi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeshapanga watumishi wa kada zote katika ngazi za mikoa ambao watafanya kazi za kuidhinisha michoro ya upangaji miji, ramani za upimaji ardhi, uthamini, umilikishaji wa ardhi pamoja na usajili wa hati na nyaraka mbalimbali. Watumishi hawa wamesharipoti kwenye vituo vyao vya kazi. Hatua inayoendelea ni kuwapanga watumishi hao kwa kuzingatia uwiano kwa kada zote za Maafisa Ardhi wakiwemo Maafisa Mipangomiji, Wapima Ardhi, Warasimu Ramani, Wathamini na Maafisa Ardhi.

Na. 369

Uzalishaji na upatikanaji wa zao la Pareto

MHE. ORAN M. NJEZA aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa soko la uhakika la zao la pareto kutokana na uhitaji mkubwa wa zao hilo duniani?

WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza mkakati wa miaka kumi (2011-2021) wa kuendeleza zao la pareto ambapo uzalishaji unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 2,400 mwaka 2019/2020 hadi tani 5,000 mwaka 2024/2025.

Aidha, ili kuongeza uzalishaji, Serikali imeviunganisha vikundi vya uzalishaji wa pareto ambapo hadi sasa jumla ya vikundi 137 vya wakulima wa pareto vimeundwa kutoka maeneo yanayolima pareto nchini ambapo kupitia vikundi hivyo ubora wa pareto umeendelea kuimarika hadi kufikia asilimia 1.3% dhidi ya wastani wa kimataifa wa asilimia 1.24.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali imeendelea kuhamasisha wakulima kujiunga na Vyama vya Msingi (AMCOs) ambapo hadi sasa jumla ya AMCOs tatu (3) zimesajiliwa na nyingine kumi (10) ziko hatua za mwisho za usajili. Pamoja na jitihada hizo zote, Serikali itaendelea kutoa elimu kwa wakulima juu ya kutumia Kanuni Bora za Kilimo cha Pareto (*Good Agricultural Practices – GAPs*) kwa ajili ya kuongeza uzalishaji na kuimarisha ubora wa pareto yenye kukidhi hitaji la soko.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuhamasisha uwekezaji na hasa uongezaji thamani ambapo kwa sasa kuna viwanda viwili vya kusindika pareto nchini ambavyo ni kiwanda cha Tanextract kilichopo Inyala Mkoani Mbeya na kiwanda cha kampuni ya "*Pyrethrum Company of Tanzania (PCT)*" kilichopo Mafinga Mkoani Iringa. Aidha, viwanda hivyo vina uwezo wa kusindika kati ya tani 2800 - 3000 kila kimoja kwa mwaka dhidi ya wastani wa uzalishaji wa tani 2,400 za pareto kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuhamasisha wakulima kulima kilimo biashara kwa kutumia kilimo cha mkataba. Vilevile, Serikali itaendelea kufanya tafiti za masoko ya ndani na ya nje ya nchi kwa kutumia Balozi zilizopo nchini

ili kuwa na uhakika wa upatikanaji wa masoko ya zao hilo la pareto.

Na. 370

Fedha kwa ajili ya Miradi ya Umwagiliaji- Igalula

MHE. MUSA R. NTIMIZI aliuliza:-

Serikali ilitengeneza andiko na ikafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina pamoja na kupata Hati ya Mazingira katika miradi mikubwa miwili ya umwagiliaji katika Kata za Goweko, Loya na Mswaki:-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha na kutekeleza miradi hii muhimu kwa wananchi wa Igalula na nchi kwa ujumla?

WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Musa Rashid Ntimizi, Mbunge wa Jimbo la Igalula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Skimu za Umwagiliaji za Loya - Miswaki na Goweko ziko kwenye Halmashauri wa Wilaya ya Uyui, Mkoani Tabora. Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kupitia iliyokuwa Ofisi ya Umwagiliaji Kanda ya Tabora kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Uyui walifanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwenye skimu za Loya - Miswaki na Goweko ili kuziendeleza.

Mheshimiwa Spika, Skimu ya Umwagiliaji ya Loya - Miswaki na Goweko ni mojawapo ya skimu za umwagiliaji zilizoainishwa kwenye Mpango Kabambe wa Umwagiliaji kwa ajili ya kuendelezwa. Kupitia mpango huu, Skimu ya Loya-Miswaki inatatarajiwa kutekelezwa katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Umwagiliaji. Aidha, awamu hiyo inatekelezwa kati ya mwaka 2018-2025 ambapo skimu 261 zitaendelezwa katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kufanya maboresho ya miundo ya kanuni, miongozo na taratibu ili skimu za umwagiliaji ziendelezwe kibiashara kwa kushirikiana na taasisi za fedha na sekta binafsi kwa utaratibu wa Kujenga, Endesha na Kabidhi (*Build Operate and Transfer-BOT*) ikiwemo Skimu za Loya, Miswaki na Goweko za Mkoani Tabora.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuchukua nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itaendelea kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Uyui ili kuhakikisha miradi tajwa inaendelezwa.

Na. 371

Fidia kwa wananchi waliopisha ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kilwa - Lindi

MHE. SELEMANI S. BUNGARA aliuliza:-

Serikali ina mpango wa kuongeza eneo la ardhi la Uwanja wa Ndege Kilwa ambapo katika mpango huo wapo wananchi waliotathminiwa maeneo yao kwa kupisha mpango huo lakini hawajalipwa:-

Je, ni sababu zipi zinazofanya wasilipwe na ni lini watalipwa fidia hiyo?

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Said Bungara, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kiwanja cha Ndege cha Kilwa ni miongoni mwa viwanja vya ndege 11 (Moshi, Songea, Musoma, Tanga, Iringa, Manyara, Singida, Kilwa Masoko, Lindi, Njombe na Simiyu) vilivyofanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ufadhili wa Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa usanifu wa kina kwa viwanja tajwa hapo juu, Serikali inatafuta fedha ili kuvifanyia ujenzi na ukarabati viwanja vyote kadri fedha inavyopatikana. Hivi sasa, tayari viwanja vitano (5) ambavyo ni Songea, Musoma, Iringa, Lake Manyara na Tanga vipo katika hatua mbalimblali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, kabla ya kuanza utekelezaji wa mradi wa ujenzi na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kilwa wananchi wanaostahili kulipwa fidia watalipwa kwa mujibu wa sheria.

Na. 372

Ongezeko la watu Lisiloendana na Rasilimali Tulizonazo

MHE. SUSAN A. J. LYIMO aliuliza:-

Je, Serikali inashauri nini kuhusu ongezeko la watu lisiloendana na rasilimali tulizo nazo?

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa chanzo kikuu cha takwimu za idadi ya watu nchini ambacho ni Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, Tanzania ilikuwa na idadi ya watu milioni 44.9. Kama mnavyofahamu, Tanzania inamiliki rasilimali ardhi yenye eneo la kilomita za mraba 947,303 (885,803 ardhi kavu na 61,500 maji) sawa na msongamano wa watu 65 kwa kila kilometa moja ya mraba kwa mwaka 2020, jambo ambalo hutoa ishara kwamba idadi kubwa ya watu nchini bado si tatizo kama Mheshimiwa Mbunge anavyoliona.

Mheshimiwa Spika, mara zote idadi ya watu imekuwa na faida zaidi kwa nchi zinazoendelea ambazo teknolojia

yake haijakua kwa kasi inayohitajika katika kuendeleza shughuli za kiuchumi ukilinganisha na nchi zilizoendelea duniani. Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliwahi kusema kuwa ili nchi iendelee inahitaji vitu vitatu ambavyo ni siasa safi, uongozi bora na watu.

Mheshimiwa Spika, kwa Tanzania rasilimali watu inaendelea kuongezeka kwa asilimia 2.7 kwa mwaka ambayo inaenda sanjari na juhudi kubwa zinazotekelezwa na Serikali za kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Spika, jitihada kubwa zinazofanyika ndani ya Serikali na ambazo zimeainishwa kwa ufasaha ndani ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021) ni pamoja na kuboresha huduma za afya, utoaji wa elimu msingi bure kwa watoto, utoaji wa pembejeo za kilimo, utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, uimarishaji wa mtandao wa usafirishaji ukijumuisha ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR, Mradi wa Kufua Umeme wa Maji Julius Nyerere - MW 2,115 kwenye maporomoko ya Mto Rufiji mradi ambao utachochea uanzishwaji wa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa ambavyo vitaajiri Watanzania wengi na kuendana na kasi ya ongezeko la idadi ya watu. Ndani ya Mpango huu mikakati mbalimbali imeelezwa kuhusu jinsi ya kukuza uchumi wa nchi ili uendane na kasi ya ongezeko la idadi ya watu. Haya yote yanayofanyika ni ishara ya nia madhubuti ya Serikali katika kutumia rasilimali watu iliyonayo nchini wakati tunaendelea na kukuza zaidi matumizi ya teknolojia na ubunifu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda nihitamishe jibu langu kwa kuwaeleza Waheshimiwa wenzangu kuwa nadharia (*theories*) zinaweza kusema idadi kubwa ya watu ni tatizo kwa rasilimali zilizopo ila kwetu sisi kama nchi ni fursa ukizingatia tuna ardhi ya kutosha na uwezo wa kuwahudumia wananchi tunao, tumezungukwa na mito, mabwawa, bandari na rasilimali nyingine nyingi. Shime tuchape kazi na tumuunge mkono Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli katika kujenga uchumi wa viwanda ambao

utatutoa hapa tulipo na kutufikisha uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Aidha, Serikali imeshaanza maandalizi ya awali kwa ajili ya zoezi la Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika mwaka 2022.

Na. 373

Mkakati wa Jeshi la Polisi katika kutumia njia za Kielektroniki

MHE. DKT. SAADA MKUYA SALUM aliuliza:-

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepiga hatua kubwa katika kuhakikisha kwamba inatumia njia za kielektroniki katika kutoa huduma zake:-

Je, Jeshi la Polisi limeweka mikakati gani katika kuhakikisha linatumia njia za kielektroniki kutoa huduma zake na hivyo kuongeza ufanisi wa utendaji wake?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Saada Salum Mkuya, Mbunge wa Welezo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa matumizi ya njia za kielektroniki katika kutoa huduma, Jeshi la Polisi lilianza kutumia njia za kielektroniki katika kutekeleza majukumu yake kuanzia mwaka 2009/2010. Baadhi ya mifumo ya kielektroniki iliyokwishatekelezwa ni pamoja na:-

1. Kuunganisha vituo vya Polisi 38 Tanzania Bara na viwili (2) Zanzibar vya daraja A na B kwenye Mkongo wa Taifa (*Optical Fiber*) ili kuruhusu mawasiliano kwa njia ya mtandao wa *internet*.
2. Kuunda mifumo ya kielektroniki. Baadhi ya mifumo iliyoundwa ni pamoja na:-
 - (i) *Loss Report*

(ii) *Traffic Management Information System - TMS*

(iii) *Human Resource Management System - HRM*

(iv) *Billing System*-mfumo wa kusimamia maduhuli mfano cheti cha tabia njema, ukaguzi wa magari, uuzaji wa mali za kuokota na kadhaalika.

3. Kuimarisha mawasiliano ya redio za mkononi (*walk talkie*) toka kwenye mfumo wa analojia kwenda katika mawasiliano ya kidijitali ambao ni salama.

Mheshimiwa Spika, mikakati ya kielektroniki inayotarajiwa kutekelezwa ni pamoja na:-

1. Kutoa elimu kwa wananchi ya jinsi ya kutumia mifumo iliyopo.

2. Kuboresha mfumo wa tozo za makosa ya Usalama Barabarani (*TMS*) kwa kununua vifaa vya kisasa kuendana na teknolojia iliyopo ya mawasiliano mfano mashine janja yenye kazi zaidi ya moja (*Androids Point of sales*).

3. Kuunganisha Mkongo wa Taifa (*Optic Fiber*) kwenye vituo 110 vilivyobaki ya daraja A na B.

4. Wataalamu wa TEHAMA wa Jeshi la Polisi wanaendelea kufanya upembuzi na usanifu wa uundaji wa mifumo ya utunzaji kumbukumbu za upelelezi na za kiintelijensia.

Na. 374

Hitaji la Boti ya Maokozi Mafia

MHE. MBARAKA K. DAU aliuliza:-

Wananchi wengi wa Mafia hutumia usafiri wa baharini kuingia na kutoka Mafia.

Je, ni lini Serikali italeta boti ya uokoaji Mafia?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, Mbunge wa Mafia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uhitaji mkubwa wa vifaa vya maokozi katika maeneo ya bahari na maziwa nchini. Hata hivyo, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji inaendelea na mazungumzo na taasisi mbalimbali za nje ya nchi ili kupatiwa vifaa mbalimbali vya zimamoto na maokozi ikiwa ni pamoja na boti za uokoaji na boti zinazotumika katika shughuli za uokoaji wakati wa mafuriko. Aidha, vifaa hivi vitakapopatikana vitagawiwa katika maeneo mbalimbali nchini yenye uhitaji ikiwemo Kisiwa cha Mafia.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaendelea kutoa elimu kwa umma kwa wamiliki na abiria wa vyombo vya usafiri majini, pamoja na kushauri kila boti kuwa na jaketi za kujiokolea (*life jackets*) na mitungi ya kuzimia moto.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaendelea kuwa na uhusiano mzuri na vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama nchini na makampuni binafsi yenye vyombo vya maokozi katika bahari na maziwa makuu kwa lengo la kushirikiana pale majanga yanapotokea.

SPIKA: Katibu!

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

**Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali
(Na. 3) 2020 (*The Written Laws (The Miscellaneous
Amendments) (No. 3) Act, 2020*)**

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

SPIKA: Ahsante sana. Sheria hiyo sasa imesomwa kwa mara ya kwanza na naipeleka moja kwa moja kwenye Kamati ya Katiba na Sheria ili waweze kuipitia na katika tarehe ya mbele kidogo wiki ijayo tutapata nafasi ya kufanya maamuzi kuhusu sheria hii. Kwa hiyo, nakuona Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Najma mjipange kuanzia leo, kesho na *weekend* hii muweze kupitia pendekezo hili la Serikali. Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:

HOJA ZA KAMATI

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Nane na Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge

SPIKA: Ahsante sana. Sasa nimkaribishe Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo aweze kuwasilisha hoja yake. Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti, karibu sana.

MHE. WILLIAM M. NGELEJA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Hii ni taarifa kuhusu uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Nane na Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha kwa niaba ya Mwenyekiti Mheshimiwa Mtemi Andrew Chenge. Kwa kuzingatia kuwa taarifa hii ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Mezani na Serikali katika Mkutano wa Kumi na Nane na Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge na ukizingatia hili ni Bunge la mwisho katika uhai wa Bunge la Kumi na Moja, naomba kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kukushukuru kwa dhati wewe binafsi kwa kuliongoza vyema Bunge hili la Kumi na Moja. Aidha, Kamati yetu inatoa pongezi kwako Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja

na Wenyeviti wote ambao pia kwa nyakati mbalimbali wamekuwa wakikusaidia vyema katika utekelezaji wa majukumu ya uendeshaji wa shughuli za Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, kupitia idhini na miongozo mbalimbali ambayo umekuwa ukiitoa kwa Kamati umetuwezesha kufanya uchambuzi wa sheria ndogo 2,601 zilizowasilishwa katika Bunge lako Tukufu, Bunge la Kumi na Moja na kupendekeza marekebisho mbalimbali katika sheria ndogo 547.

Aidha, kufuatia uchambuzi huo, Kamati imeweza kuwasilisha Bungeni taarifa za uchambuzi wa sheria ndogo hizo kwa kadri ambavyo ilikupendeza na ukatoa maelekezo hayo.

Mheshimiwa Spika, namna ambavyo Kamati imetekeleza majukumu yake. Kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge lako Tukufu kufuatilia ipasavyo utekelezaji wa madaraka yake ya kutunga sheria yaliyokasimiwa kwa mamlaka mbalimbali, naomba kubainisha mambo yaliyozingatiwa na Kamati wakati wa uchambuzi wa sheria ndogo zilizowekwa mezani kama ifuatavyo:-

(i) Kujiridhisha iwapo sheria ndogo husika inakiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(ii) Kujiridhisha iwapo sheria ndogo husika inavuka mipaka au kwenda kinyume na masharti ya sheria inayotoa mamlaka ya kutunga sheria ndogo au sheria nyingine yoyote.

(iii) Kujiridhisha iwapo sheria ndogo husika imezingatia misingi bora ya uandishi wa sheria (*drafting principles*).

(iv) Kujiridhisha iwapo sheria ndogo husika inakiuka misingi ya haki za kibinadamu.

(v) Kujiridhisha iwapo sheria ndogo inaendana na uhalisia wa mambo ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake, hali ya uchumi wa walengwa na viwango vya adhabu na *fine*.

(vi) Kujiridhisha kuhusu maudhui ya jumla ya sheria ndogo pamoja na makosa ya uandishi na uchapaji.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimeshaeleza katika maelezo ya awali kuwa taarifa hii inajumuisha uchambuzi wa sheria ndogo za Mkutano wa Kumi na Nane na Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge. Sehemu zinazofuata zitaonyesha uchambuzi wa baadhi ya sheria ndogo za Mkutano wa Kumi na Nane na sheria ndogo za Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwakatika Mkutano wa Kumi na Nane wa Bunge. Mnamo tarehe 4 Februari, 2020, Serikali iliwasilisha mezani nakala za Magazeti ya Serikali na viambatisho vyake zikiwemo jumla ya sheria ndogo 228 kwa mujibu wa kifungu cha 38(1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 na Kanuni ya 37(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Kamati ilichambua na kubaini dosari mbalimbali katika sheria ndogo 22 zilizo chini ya Wizara ya Maji, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi kamili wa sheria ndogo hizo umeonyeshwa katika jedwali la uchambuzi lililoambatanishwa katika taarifa ya Kamati ambayo kimsingi ilishawasilishwa tayari na iko kwenye mfumo wetu wa kawaida huu wa kidigitali na kila mmoja anaweza kuipakua. Kwa minajili ya kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuhusu uchambuzi uliofanyika, baadhi ya dosari zilizobainika katika kanuni hizo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ndogo kwenda kinyume na sheria mama au sheria nyingine za nchi. Katika hili, Kamati ilifanya uchambuzi wa sheria ndogo za ada na ushuru za Halmashauri ya Mkinga zilizotungwa mwaka 2019 ambazo zimetungwa chini ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290 na kubaini zinakwenda kinyume na Sheria Mama. Dosari hiyo iliyobainika katika Sehemu ya Nne ya Jedwali la

Kwanza inayoweka sharti la malipo ya ada na ushuru wa kiwango cha asilimia 5 ya bei ya kununulia kwa mazao ya korosho na mazao mengine ambayo hayajatajwa katika sehemu ya nne kinyume na Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290 ambayo imeweka kiwango cha asilimia 3 kwa mazao yote na asilimia 5 kwa mazao ya misitu.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha ada kinachowekwa katika Sehemu ya Nne ya Jedwali la Kwanza kinakwenda kinyume na masharti yaliyowekwa na kifungu cha 36(1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 ambacho kinaelekeza kwamba sheria ndogo haipaswi kwenda kinyume na vifungu vya sheria mama vinavyoianzisha au sheria yoyote ya nchi. Hivyo, kwa mantiki ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria kiwango kinachowekwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii ni batili kwa kiwango inachokinzana na Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sheria ndogo kutozingatia misingi ya uandishi wa sheria kwa maana ya *drafting principles*. Kamati ilifanya uchambuzi wa sheria ndogo ya *The Local Government Authorities Rating, Collection of Property Rates Regulations* za mwaka 2020 zilizoanzishwa chini ya Sheria ya *The Local Government Authority Rating Act*, Sura 289. Katika uchambuzi huo, Kamati imebaini dosari za uandishi ambapo Kanuni za 9(1), 10(3), 11(1) zinaonyesha uwepo wa *assessment notice form, demand notice form* na *installment payment agreement form* katika jedwali la kanuni hizi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, jedwali halijaonyesha fomu hizo zinazorejewa na kanuni tajwa jambo ambalo linasababisha sheria ndogo hii kutokukamilika na hivyo kuleta changamoto ya namna ya utekelezaji wa baadhi ya maeneo ya sheria. Ni vyema waandishi wa sheria ndogo wakazingatia masharti ya kifungu cha 25(2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria ambacho kinataja majedwali kuwa ni sehemu ya sheria. Hivyo, ni vyema kuhakikisha majedwali yanaandikwa kwa usahihi ili kuweka utaratibu mzuri wa utekelezaji wa vifungu vya sheria.

Mheshimiwa Spika, sheria ndogo kuwa na makosa ya uandishi katika majedwali na kutorojea kanuni sahihi, kurejea kanuni ambazo hazipo, kutorejea kabisa kanuni na maudhui ya jedwali kutofautiana na vifungu. Katika hili, makosa ya kiuandishi yamebainika katika Kanuni za Kudumu za Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga ambazo ni za mwaka 2019 ambazo zimetungwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka za Wilaya, Sura ya 287. Jedwali la Kwanza limerejea kuanzishwa chini ya Kanuni ya 42(3) ambayo haipo katika kanuni hizi.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba rejea sahihi iliyopaswa kuwekwa katika jedwali hili ni Kanuni ya 44(3) ambayo ndiyo chenye maudhui sahihi ya Jedwali la Kwanza la sheria ndogo hizi. Ni vyema uandishi wa majedwali katika sheria uzingatie kurejea kanuni sahihi zinazoanzisha majedwali haya kwa kuwa majedwali hufafanua zaidi masharti ya utekelezaji wa kanuni husika katika sheria ndogo.

Mheshimiwa Spika, sheria ndogo kutoendana na uhalisia wa mambo ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake, hali ya uchumi wa walengwa na viwango vya adhabu na *fine*. Katika hili, Kamati imebaini masharti yasiyo na uhalisia katika utekelezaji wake. Mfano ni Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe za mwaka 2019 zilizotungwa chini ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290. Jedwali la Kwanza linaweka sharti la malipo ya ushuru wa shilingi laki moja kwa gari lenye ujazo wowote wa mizigo ya mazao au bidhaa mbalimbali kushusha mizigo na mifugo katika masoko ya maeneo ya vivuko. Sharti hili halina uhalisia kwa kuwa halizingatii ukweli kwamba magari ya kupakia mizigo yana uzito tofauti, hata ujazo wa mizigo unatofautiana kati ya gari moja na gari lingine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge. Mnamo tarehe 8 Aprili, 2020, Serikali iliwasilisha mezani nakala za Magazeti ya Serikali na viambatisho vyake zikiwemo jumla ya sheria ndogo 188 kwa mujibu wa kifungu

cha 38(1) cha Tafsiri ya Sheria, Sura ya Kwanza na Kanuni ya 37(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua na kubaini dosari mbalimbali katika sheria ndogo sita zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano; Wizara ya Katiba na Sheria; na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Uchambuzi kamili wa sheria ndogo umeoneshwa katika Jedwali la Uchambuzi lililoambatishwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kwa minajili ya kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuhusu uchambuzi uliofanyika baadhi ya dosari zilizobainika katika kanuni hizo ni kama ifuatavyo na nyingi zinajirudia kwamba baadhi yake sheria ndogo zimekwenda kinyume na sheria mama au sheria nyingine za nchi. Katika hili, dosari imebainika katika Sheria ya *The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Code of Conduct for Investors Natural Wealth and Resources Regulations* za mwaka 2020 zilizotungwa chini ya Sheria ya *The Natural Wealth Resources (Permanent Sovereignty) Act*, Sura 449 na Kanuni ya 10 ambayo imebainisha makatazo tisa ya ubaguzi dhidi ya mwajiriwa ambayo kimsingi ni machache ikilinganishwa na makazo ambayo yameainishwa katika kifungu cha 7(4) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura ya 366 ambacho kimeainisha makatazo 15 ya ubaguzi dhidi ya mwajiriwa. Katika hili, Kamati inaona ni vyema sheria ndogo zinapotungwa zizingatie masharti ambayo tayari yamewekwa na sheria mama au sheria nyingine za nchi ili kuepuka kukinzana kwa sheria ambapo ni kinyume na kifungu cha 36(1) cha Sheria ya Tafsiri za Sheria Sura ya 1. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu sheria ndogo kutokuzingatia misingi bora ya uandishi wa sheria. Katika hili, sheria ndogo iliyobainika kuweka masharti yasiyo na uhalisia ni *The Electronic and Postal Communication Simcard Registrations Regulation* za mwaka 2020 ambayo imetungwa chini ya *The Electronic and Postal Communications Act*, Sura 306. Kamati imebaini kuwa kwa namna ambavyo imeandikwa inazuia umiliki wa laini ya simu zaidi ya moja kutoka katika kampuni moja ya simu. Kanuni ya 18(1)

imeweka masharti ya idadi ya kadi za simu zinazopaswa kumilikiwa na mtu, kampuni au taasisi ambapo kwa mtu binafsi hatapaswa kumiliki zaidi ya laini ya simu ama *simcard* moja kutoka kampuni moja ya simu kwa matumizi ya huduma ya kupiga, kutuma ujumbe mfupi wa maneno na matumizi ya mtandao data. Iwapo ni kampuni au taasisi basi hazitapaswa kumiliki zaidi ya kadi ya simu 30 kutoka katika kampuni moja ya simu kwa matumizi ya huduma ya kupiga, ujumbe mfupi wa maneno na matumizi ya mtandao yaani *data*.

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu inaona kuwa ni vyema uandishi wa kanuni hii ukaonesha kuwa haiweki katazo la umiliki wa laini nyingi za simu kwa kadri mtu, kampuni au taasisi itaona nafaa kufanya hivyo. Aidha, Kamati yetu inapendekeza kuwa Kanuni ya 18(3) inayotoa fursa ya kuwasilisha maombi kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ya kumiliki laini za ziada tofauti na ilivyoainishwa kwa mujibu wa Kanuni hizi ifanyiwe marekebisho ili iainishe utaratibu wa namna ya kuwasilisha maombi ya laini za ziada kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania pamoja na utaratibu wa kuzingatia iwapo mwombaji hataridhika na uamuzi wa Mamlaka hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri ni vyema katika siku za usoni sharti hili la kuweka idadi ya umiliki wa laini za simu likaondolewa kwa kuwa wamiliki wa laini hizo za simu watakuwa wamezingatia taratibu zote za usajili badala yake Wizara na vyombo husika zitumie mifumo iliyopo kudhibiti namna bora ya matumizi ya laini hizo za simu zinazotumika pasipo kuweka ukomo wa idadi wa laini zinazopaswa kumilikiwa na mtu, kampuni ama taasisi. Hatua hii itawezesha kupanua wigo wa makampuni kupata mapato mengi yatokanayo na kuwa na wateja wengi wanaotumia huduma zake vilevile kutanua wigo wa Serikali kukusanya zaidi mapato ya kodi mbalimbali zitokanazo na matumizi ya mitandao ya simu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sheria ndogo kutokuendana na uhalisia wa mambo ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake. Katika hili, uchambuzi wa Kamati yetu

umebaini kuwa baadhi ya Kanuni za Wizara zimeweka masharti yasiyokuwa na uhalisia ambayo yanaweza kuleta madhara katika utekelezaji wake. Kanuni hizo ni *The Transport Licensing Public Service Vehicles Regulations* ya mwaka 2020 ambazo zimetungwa chini ya Sheria ya *The Transport Licensing Act*, Sura 317 ambapo Kanuni ya 26 inaweka sharti kwa mwenye leseni ya kutoa huduma ya usafiri wa mabasi ya shule kuwa na dereva mwenye umri usiopungua miaka 35 na isiyozidi 60. Kamati ina maoni kwamba sharti la umri lililowekwa kwa mujibu wa Kanuni hii halina uhalisia kwa kuwa udereza hauzingatii umri tu ulioainishwa bali hutegemea uzoefu wa dereva husika katika kuendesha vyombo vya usafiri. Hivyo, Kamati inashauri Kanuni iboreshwe kwa kuongeza sharti la kumtaka dereva mwenye leseni ya daraja la kuendesha mabasi ya shule awe pia na uzoefu wa kuendesha magari ya shule usiopungua miaka 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu sheria ndogo kukiuka misingi ya haki za binadamu. Katika hili, uchambuzi wa Kamati yetu umebaini kuwepo kwa sheria ndogo zinazokwenda kinyume na haki za binadamu. Sheria ndogo hizo ni pamoja na *The Transport Licensing Public Service Vehicles Regulations* ya mwaka 2020 iliyotungwa chini ya Sheria ya *Transport Licensing Act*, Sura ya 317. Kanuni ya 28(4) inatoa fursa kwa Mamlaka kusitisha leseni ya mtoa huduma ya usafirishaji pasipo kutoa fursa ya kumsikiliza mwenye leseni.

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati yetu ni kwamba maudhui ya kanuni hii ni kinyume na misingi ya haki za asili ambazo zinaweka sharti la mtu kusikilizwa kabla ya kupewa adhabu. Hivyo, Kamati inaona ni vyema kanuni zikaweka bayana mienendo na matukio yanayoweza kupelekea usitishwaji wa leseni pasipo kumsikiliza mtoa huduma. Hii itasaidia kuondoa uwezekano wa matumizi mabaya ya kanuni hii na kupelekea kusitishwa ghafla kwa huduma ya usafiri, kuleta usumbufu kwa watumiaji wa huduma ya usafiri husika pamoja na kuleta athari mbalimbali zitokanazo na uwekezaji uliofanyika katika huduma husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu sheria ndogo kuwa na makosa ya uandishi katika majedwali. Kamati pia imebaini kasoro mbalimbali katika majedwali yaliyopo katika sheria ndogo. Kasoro hizo zimebainika katika Sheria Ndogo za *Natural Wealth and Resources Contract (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Regulations* za mwaka 2020 iliyotungwa chini ya Sheria ya *The Natural Wealth Resources Contract (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act*, Sura ya 450 ambapo fomu NWR fomu namba 3 iliyo katika Jedwali la Tatu lina makosa ya uandishi kwa kutumia maneno yasiyo na muktadha unaoendana na kanuni hii ambapo maneno *General Assembly* yametumika badala ya maneno *National Assembly* ambayo ndiyo yaliyokusudiwa katika fomu hii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya jumla. Kuhusu uandishi wa sheria ndogo. Katika hili, Kamati inashauri mamlaka zilizokasimiwa jukumu la utungaji wa sheria ndogo kuepuka kutunga sheria ndogo zilizoweka masharti ya jumla katika baadhi ya vifungu na badala yake zitunge sheria ndogo zinazoweka vifungu vinavyofafanua kwa kina namna ya utekelezaji wa masharti mbalimbali yaliyowekwa na sheria mama.

Mheshimiwa Spika, utoaji wa elimu kuhusu masuala ya sheria ndogo na ushirikishwaji wa wadau. Kamati inashauri kuwa ni vyema Wizara zikaendelea na programu za utoaji wa elimu kwa umma na kushirikisha wadau kwa karibu inapotokea kuna utungwaji wa sheria ndogo mpya zinazolenga kuweka utaratibu wa namna ya kusimamia sekta fulani.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano wa taasisi ama Wizara na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kamati inazishauri mamlaka zilizopewa jukumu la kutunga sheria ndogo kufanya kazi kwa karibu na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakati wa utungaji wa sheria ndogo hizi ili kupata ushauri mzuri wa namna bora ya uandishi wa sheria ndogo.

Mheshimiwa Spika, mamlaka kutotekeleza maeneo ya sheria mpaka pale ambapo marekebisho ya maeneo haya yamefanyika. Katika hili, Kamati inashauri kwamba mamlaka mbalimbali ambazo sheria ndogo zake zimebainika kuwa na vifungu vyenye dosari mbalimbali kusitisha utekelezaji wa vifungu hivyo hadi mabadiliko yatakapofanyika kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati. Hii itasaidia kuondoa athari mbalimbali zinazoweza kutokea kwa wanaoguswa na sheria hizo kutokana na utekelezwaji wake.

Mheshimiwa Spika, kufanya marekebisho katika sheria ndogo zilizobainika kuwa na dosari. Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kuzifanyia marekebisho sheria ndogo zote zenye dosari. Baada ya marekebisho hayo kufanyika na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali, sheria ndogo hizo ziwasilishwe Bungeni kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, hoja yetu kuhusu sheria ndogo kukinzana na masharti ya sheria mama au sheria nyingine za nchi ni kama ifuatavyo:-

KWA KUWA baadhi ya sheria ndogo zilizofanyiwa uchambuzi na Kamati zilibainika kuwa na vifungu vilivyokinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi;

NA KWA KUWA kukinzana huko ni kwenda kinyume na masharti ya kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinachotoa sharti kwa sheria ndogo kutokwenda kinyume na masharti ya sheria mama;

Na KWA KUWA kukinzana huko kunaifanya kanuni husika kuwa ni batili kwa kiwango kilichokinzana;

KWA HIYO BASI Bunge linaazimia kwamba Wizara zinazohusika zifanye marekebisho katika sheria ndogo hizo ili kuondoa vifungu vinavyokwenda kinyume na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi.

Mheshimiwa Spika, hoja kuhusu sheria ndogo kuwa na dosari ya uandishi wa majedwali ikilinganishwa na vifungu vya sharia ni kama ifuatavyo:-

KWA KUWA katika uchambuzi wa Kamati imebainika kuwa baadhi ya sheria ndogo zina dosari mbalimbali katika majedwali kuhusu vifungu vinavyoanzisha majedwali husika;

NA KWA KUWA kwa mujibu wa kifungu cha 25(2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinabainisha kwamba majedwali ni sehemu ya sheria;

KWA HIYO BASI Bunge linaazimia kwamba Wizara ambazo sheria ndogo zake zimebainika kuwa na dosari katika majedwali zifanyiwe marekebisho ili kuondoa dosari hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu sheria ndogo kutozingatia misingi ya uandishi wa sheria yaani *drafting principles*, hoja ni kama ifuatavyo:-

KWA KUWA katika uchambuzi wa Kamati imebainika kwamba baadhi ya sheria ndogo zina dosari mbalimbali za kiuandishi;

NA KWA KUWA dosari hizo zimesababisha mantiki na madhumuni yaliyokusudiwa katika vifungu husika kutofikiwa na hivyo kuleta changamoto katika utekelezaji wake;

KWA HIYO BASI Bunge linaazimia kwamba Wizara ambazo sheria ndogo zake zimebainika kuwa na dosari za kiuandishi zifanye marekebisho ili kuondoa dosari hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja kuhusu sheria ndogo kutozingatia masharti ya haki za binadamu ni kama ifuatavyo:-

KWA KUWA uchambuzi wa Kamati umebaini uwepo wa sheria ndogo zenye vifungu vinavyokiuka misingi ya haki za binadamu;

NA KWA KUWA utekelezaji wa vifungu hivyo unaweza kusababisha kukosekana kwa haki za msingi kwa walengwa wa sheria husika;

KWA HIYO BASI Bunge linaazimia kwamba Wizara ambazo sheria ndogo zake zimebainika kuwa na dosari katika vifungu vinavyokiuka misingi ya haki za binadamu zifanye marekebisho ili kuondoa dosari hizo.

Mheshimiwa Spika, hoja kuhusu sheria ndogo kuweka masharti yasiyo na uhalisia ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake, hali ya uchumi wa walengwa na viwango vya adhabu na faini ni kama ifuatavyo:-

KWA KUWA katika uchambuzi wa Kamati imebainika kuwepo kwa dosari zilizoweka vifungu vyenye masharti yasiyo na uhalisia;

NA KWA KUWA dosari hizo zinaweza kusababisha ugumu katika utekelezaji wake na hivyo kukandamiza wanaolengwa na sheria ndogo husika;

KWA HIYO BASI Bunge linaazimia kwamba Wizara ambazo sheria ndogo zake zimebainika kuwa na dosari katika vifungu vyenye masharti yasiyo na uhalisia zifanye marekebisho ili kuondoa dosari hizo.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani za dhati kwako binafsi na Bunge lako Tukufu kwa kuweka utaratibu wa Taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuwasilishwa katika Bunge lako Tukufu kwa kadri ambavyo ulielekeza na ikafanyika. Ni matumaini yetu kama Kamati kwamba utaratibu huu utakuwa endelevu na hivyo kuchangia katika maendeleo ya nchi yetu kwa kuwa masuala mengi yanayoibuliwa kutokana na uchambuzi wa

sheria ndogo kwa kiasi kikubwa yanagusa maisha ya kila siku ya wananchi wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee, Kamati inaomba kumshukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu kwa kuendelea kuweka utaratibu mzuri ambao uliwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa kipindi chote cha Bunge la Kumi na Moja.

Aidha, sisi Kamati tunawashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu pamoja na watendaji wa taasisi zilizo chini ya Wizara husika waliofika mbele ya Kamati yetu katika Bunge hili la Kumi na Moja na kujibu hoja zilizoibuliwa na Kamati. Kupitia majadiliano yenye tija katika vikao hivyo imesababisha kufanyika marekebisho mbalimbali katika sheria ndogo zilizobainika kuwa na dosari.

Mheshimiwa Spika, vilevile kipekee kabisa, pamoja na mengine, tunawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa katika mikutano iliyotangulia ya Bunge la Kumi na Moja pamoja na kuchambua sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Nane na Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge na hatimaye kuandaa taarifa hii. Katika hili, tunalishukuru pia Bunge lote kwa sababu kwa namna moja ama nyingine wametusaidia kufanikisha kazi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuwa kazi ya uchambuzi wa sheria ndogo ni ngumu kwa kuwa sheria zinazowasilishwa Bungeni huwa ni nyingi lakini pasipo kuangalia hilo, Wajumbe wa Kamati hii wameifanya kazi hii kwa moyo na juhudi ya hali ya juu na hatimaye kuweza kuchambua sheria ndogo zote zilizowasilishwa katika Bunge la Kumi na Moja. Kwa heshima kubwa naomba majina ya waliohusika pamoja na taarifa hii yasomwe kama ambavyo yanaonekana kwenye taarifa rasmi iliyowasilishwa na ambayo Waheshimiwa Wabunge wanaweza kuipakua.

Mheshimiwa Spika, sisi Wanakamati pia tunaendelea kuwashukuru watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya ugozi mahiri wa Ndg. Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge, kwa ushirikiano waliotupatia Kamati hii na kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, tunamshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Michael Chikokoto, akisaidiwa na Ndg. Gerald Magili, Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Kamati za Bunge kwa usimamizi mzuri wa shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, tunaendelea kuwashukuru Makatibu wa Kamati yetu, Ndg. Angela Shekifu, Ndg. Stanslaus Kagisa, Ndg. Mkuta Masoli, wakisaidiwa na mtu maarifu sana, mtu bigwa, Ndg. Paul Chima, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, naomba kutoa hoja.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, naafiki.

**TAARIFA KUHUSU UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO
ZILIZOWASILISHWA KATIKA MKUTANO WA KUMI NA NANE NA
MKUTANO WA KUMI NA TISA WA BUNGE - KAMA
ILIVYOWASILISHWA BUNGENI**

1.0 UTANGULIZI

1.1 Maelezo ya Awali

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa Taarifa hii ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Mezani na Serikali katika Mkutano wa Kumi na Nane na Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge ni ya mwisho katika uhai wa Bunge la Kumi na Moja, hivyo nichukue fursa hii kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kukushukuru kwa dhati wewe binafsi kwa kulingoza vema Bunge hili la Kumi na Moja. Aidha, Kamati inatoa pongezi kwa Mheshimiwa Naibu Spika wa Bunge na Waheshimiwa

Wenyeviti wa Bunge ambao pia kwa nyakati mbalimbali wamekuwa wakikusaidia vema katika utekelezaji wa majukumu ya uendeshaji wa shughuli za Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, kupitia idhini na miongozo mbalimbali ambayo umekuwa ukitoa kwa Kamati, imeiwezesha Kamati kufanya uchambuzi wa Sheria Ndogo **Elfu Mbili Mia Sita na Moja (2,601)** zilizowasilishwa katika Bunge la Kumi na Moja na kupendekeza marekebisho mbalimbali katika **Sheria Ndogo Mia Tano Arobaini na Saba (547)**. Aidha, kufuatia uchambuzi huo Kamati imeweza kuwasilisha Bungeni Taarifa za Uchambuzi wa Sheria Ndogo hizo.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hizo zimewezesha Kamati kutoa ushauri mbalimbali kuhusu Sheria Ndogo zilizochambuliwa pamoja na Sheria Ndogo nyingine ambazo zinatumika ambapo Serikali imekuwa ikifanyia kazi Maoni na Mapendekezo na kuondoa dosari zilizobainika.

1.2 Madaraka ya Kutunga Sheria

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 64 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, imelipa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mamlaka yote ya kutunga Sheria juu ya mambo yote ya Muungano na yasiyo ya Muungano yahusuyo Tanzania bara. Aidha, Ibara ya 97 ya Katiba imeweka utaratibu ambao unapaswa kuzingatiwa na Bunge katika kutekeleza madaraka yake ya kutunga Sheria.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mamlaka lililonayo Bunge la kutunga Sheria, kwa hali halisi Bunge halina muda wa kutosha wa kutunga Sheria kuhusu masuala yote ambayo utekelezaji wake unahitaji uwepo wa Sheria. Kutokana na hali hiyo ndiyo maana Ibara ya 97 (5) ya Katiba inalipa Bunge uwezo wa kukasimu madaraka yake ya kutunga Sheria kwa mtu yeyote au idara yoyote ya Serikali.

1.3 Udhibiti wa Kibunge wa Sheria Ndogo

Mheshimiwa Spika, Udhibiti wa Kibunge wa Sheria Ndogo (*Parliamentary Control Over Subsidiary Legislation*) ni utaratibu wa kawaida katika Mabunge ya nchi za Jumuiya

ya Madola. Utaratibu huu unalenga kuliwezesha Bunge kujiridhisha kikamilifu kuhusu utekelezaji wa madaraka ya kutunga sheria lililoyakasimu kwa mamlaka nyingine. Katika jukumu lake la udhibiti, Bunge huzingatia masharti ya Sheria Mama iliyoruhusu utungwaji wa Sheria Ndogo husika na misingi mingine iliyowekwa na Sheria zilizotungwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, dhana ya udhibiti wa Sheria Ndogo pia limeelezwa vizuri katika Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 (*The Interpretation of Laws Act, Cap 1 R.E. 2002*) ambayo imeweka masharti maalumu yanayolipa Bunge la Tanzania mamlaka ya udhibiti wa Sheria Ndogo zinazotungwa na Serikali pamoja na vyombo vyake.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa kufanya Udhibiti wa Utungaji wa Sheria Ndogo, Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge ikisomwa kwa pamoja na Nyongeza ya Nane ya Kanuni hizo imeanzisha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kama ilivyo kwa Mabunge mengine katika Nchi za Jumuiya ya Madola.

Kamati hii imepewa majukumu kwa mujibu wa Kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 ambayo ni, kuchambua Sheria Ndogo ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi.

1.4 Namna ambavyo Kamati inatekeleza majukumu yake

Mheshimiwa Spika, wajibu wa msingi wa Kamati kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, kama ambavyo imeelezwa awali, ni kufanya uchambuzi wa Sheria Ndogo ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge lako tukufu kufuatilia ipasavyo utekelezaji wa madaraka yake ya kutunga sheria yaliyokasimiwa kwa mamlaka mbalimbali, naomba kubainisha mambo yanayozingatiwa na Kamati

wakati wa uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowekwa Mezani. Mambo hayo ni:-

i) Kujiridhisha iwapo Sheria Ndogo husika inakiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

ii) Kujiridhisha iwapo Sheria Ndogo husika inavuka mipaka au kwenda kinyume na masharti ya Sheria inayotoa mamlaka ya kutunga Sheria Ndogo au Sheria nyingine yoyote;

iii) Kujiridhisha iwapo Sheria Ndogo husika imezingatia misingi bora ya uandishi wa Sheria (*drafting principles*);

iv) Kujiridhisha iwapo Sheria Ndogo husika inakiuka misingi ya haki za binadamu;

v) Kujiridhisha iwapo Sheria Ndogo inaendana na uhalisia wa mambo ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake, hali ya uchumi wa walengwa na viwango vya adhabu na faini; na

vi) Kujiridhisha kuhusu maudhui ya jumla ya Sheria Ndogo pamoja na makosa ya uandishi na uchapaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilisha uchambuzi wake kwa kuzingatia masuala yaliyotajwa, Kamati hubaini hoja mbalimbali zinazolenga kupata ufafanuzi katika maeneo ya Sheria Ndogo zenye dosari. Hoja hizo huwasilishwa Serikalini kwa lengo la kupata ufafanuzi, kupendekeza marekebisho au kufutwa kwa kifungu chochote ambacho kina dosari zilizobainishwa na Kamati. Baada ya hoja hizo kuwasilishwa, Wizara zinazoguswa na hoja zinazoibuliwa na Kamati, huwajibika kufika mbele ya Kamati na kutoa maelezo kuhusiana na Sheria Ndogo zilizo chini yao.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nilieleza hapo awali kuwa Taarifa hii inajumuisha Uchambuzi wa Sheria Ndogo za Mkutano wa Kumi na Nane na Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge. Sehemu zinazofuata zinaonesha baadhi ya uchambuzi wa Sheria Ndogo za Mkutano wa Kumi na Nane na Sheria Ndogo za Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge.

2.0 UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA KATIKA MKUTANO WA KUMI NA NANE WA BUNGE

Mnamo tarehe 4 Februari, 2020 Serikali iliwasilisha Mezani nakala za Magazeti ya Serikali na viambatisho vyake zikiwemo jumla ya Sheria Ndogo Mia Mbili Ishirini na Nane (228) kwa mujibu wa Kifungu cha 38(1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura 1 na Kanuni ya 37(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Sheria Ndogo hizo zimegawanyika katika makundi yafuatayo:-

- a) Sheria Ndogo za Halmashauri (*By - Laws*) – 43;
- b) Kanuni za Wizara (*Regulations*) – 26;
- c) Amri (*Orders*) - 146);
- d) Matangazo (*Notices*) – 8;
- e) Kanuni za Tasisi (*Rules*) – 2 ; na
- f) Matamko (*Proclamations*) – 3.

Mheshimiwa Spika, katika mchanganuo wa Sheria Ndogo ulioainishwa, Kamati ilichambua na kubaini dosari mbalimbali katika Sheria Ndogo Ishirini na Mbili (22) zilizo chini ya Wizara zifuatazo:-

- a) Wizara ya Maji;
- b) Ofisi ya Rais – TAMISEMI;
- c) Wizara ya Fedha na Mipango; na
- d) Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, baada ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo hizo, Kamati imetoa maoni na ushauri kwa lengo la kuboresha maudhui ya Kanuni hizo kama zinavyoonekana katika **JEDWALI LA UCHAMBUZI** lililoambatishwa katika Taarifa ya Kamati. Kwa minajili ya kulitaarifu Bunge kuhusu uchambuzi uliofanyika, baadhi ya dosari zilizobainika katika Kanuni hizoni kama ifuatavyo:-

- a) **Sheria Ndogo kwenda kinyume na Sheria Mama au Sheria nyingine za Nchi.**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa, baadhi ya Sheria Ndogo zilizotungwa na Wizara (*Regulations*) zinakwenda

kinyume na masharti yaliyowekwa na Sheria Mama au na Sheria Nyingine za Nchi. Kifungu cha 36 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria ambacho kinabainisha kwamba, Sheria Ndogo yoyote haipaswi kukiuka masharti ya Sheria ya Bunge inayotoa mamlaka ya kutungwa kwake au Sheria nyingine yoyote.

Mheshimiwa Spika, Sheria Ndogo zilizobainika kuwa na dosari ya kwenda kinyume na Sheria Mama na Sheria nyingine za Nchi ni *The Water Supply, Regulations 2019* ambazo zimetungwa chini Sheria ya *The Water Supply and Sanitation Act Na. 5 ya Mwaka 2019* ambapo uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Kanuni haijaonesha imetungwa chini ya Kifungu kipi cha Sheria Mama.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Kanuni hii inaenda kinyume na masharti yaliyowekwa katika **Kifungu cha 36(1)** cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya 1 (*Intepretation of Laws Act*) ambacho kinaelekeza kwamba, Sheria Ndogo haipaswi kwenda kinyume na vifungu vya Sheria Mama vinavyoianzisha au Sheria yoyote ya Nchi. Hivyo kwa mantiki ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Kanuni hii ni batili kwa kukosa kifungu kinachoianzisha.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilifanya uchambuzi wa **Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga, 2019** ambayo imetungwa chini Sheria ya **Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290** na kubaini inakwenda kinyume na Sheria Mama. Dosari hiyo ilibainika katika **Sehemu ya Nne ya Jedwali la Kwanza** inayoweka sharti la malipo ya ada na ushuru kwa kiwango cha 5% ya bei ya kununulia kwa mazao ya korosho na mazao mengine ambayo hayajatajwa katika Sehemu ya Nne, kinyume na Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, 290 ambayo imeweka kiwango cha 3% kwa mazao yote na 5% kwa mazao ya misitu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kiwango cha Ada kinachowekwa katika **Sehemu ya Nne ya Jedwali la Kwanza** kinakwenda kinyume na masharti yaliyowekwa na **Kifungu cha 36(1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya 1**

(Interpretation of Laws Act) ambacho kinaelekeza kwamba, Sheria Ndogo haipaswi kwenda kinyume na vifungu vya Sheria Mama vinavyoianzisha au Sheria yoyote ya Nchi. Hivyo kwa mantiki ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Kiwango kinachowekwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii ni batili kwa kiwango inachokinzana na **Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290**.

b) **Sheria Ndogo kutozingatia misingi ya uandishi wa Sheria (Drafting Principles)**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa Sheria Ndogo ya **The Local Government Authorities (Rating) (Collection of Property Rates) Regulations, 2020** zilizoanzishwa chini ya Sheria ya **Local Government Authorities (Rating) Act, (Sura 289)**. Katika uchambuzi huo Kamati imebaini dosari za uandishi ambapo **Kanuni ya 9(1), 10 (3) na 11(1)** zinaonesha uwepo wa **Assesment Notice Form, Demand Notice Form na Installment Payment Agreement Form** katika Jedwali la Kanuni hizi. Hata hivyo Jedwali halijaonesha fomu hizo zinazorejewa na Kanuni tajwa jambo ambalo linasababisha Sheria Ndogo hii kutokamilika na hivyo kuleta changamoto ya namna ya utekelezaji wa baadhi ya maeneo ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, ni vema waandishi wa Sheria Ndogo wakazingatia masharti ya Kifungu cha 25 (2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria ambacho kinataja Majedwali kuwa ni sehemu ya sheria, hivyo ni vema kuhakikisha Majedwali yanaandikwa kwa usahihi ili kuweka utaratibu mzuri wa utekelezaji wa vifungu vya Sheria.

c) **Sheria Ndogo kuwa na makosa ya uandishi katika Majedwali (Kutorejea Kanuni sahihi, kurejea Kanuni ambazo hazipo, kutorejea kabisa Kanuni na Maudhui ya Jedwali kutofautiana na Vifungu)**

Mheshimiwa Spika, Makosa ya kiuandishi yamebainika katika Kanuni za Kudumu za Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga, 2019, ambazo zimetungwa chini ya **Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) (Sura ya 287)**. Kama zilivyo sheria

nyingine, sheria hii pia ina Majedwali ambayo yanaweka ufafanuzi wa Kanuni mbalimbali katika Sheria Ndogo hii. Hata hivyo Kamati imebaini dosari katika rejea za Kanuni zinazoanzisha majedwali. Kwa mfano, **Jedwali la Kwanza** limerejea kuanzishwa chini ya **Kanuni ya 42(3)** ambayo haipo katika Kanuni hizi. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba rejea sahihi iliyopaswa kuwekwa katika Jedwali hili ni Kanuni ya 44(3) ambayo ndiyo chenye maudhui sahihi ya Jedwali la la Sheria Ndogo hizi.

Mheshimiwa Spika, ni vema uandishi wa majedwali katika sheria uzingatie kurejea Kanuni sahihi zinazo anzisha majedwali husika, kwa kuwa majedwali hufafanua zaidi masharti ya utekelezaji wa Kanuni husika katika Sheria Ndogo. Hivyo kwa kutorejea vifungu sahihi sio tu inaondoa maana ya masharti ya Kifungu cha 25 (2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria ambacho kinatambua majedwali kuwa ni sehemu ya sheria, bali pia inaleta changamoto katika usomaji mzuri wa sheria husika.

d) **Sheria Ndogo kutoendana na uhalisia wa mambo ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake, hali ya uchumi wa walengwa na viwango vya adhabu na faini**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini uwepo wa masharti yasiyo na uhalisia katika **Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Monduli, 2019** zilizotungwa chini ya **Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) (Sura 287)** zimetungwa chini ya kifungu cha 153. **Kifungu cha 6** kinaweka katazo kwa mtu yeyote kupanda mazao au mimea mirefu katika maeneo ya mjini.

Mheshimiwa Spika, Masharti ya Sheria Ndogo hii si halisia kwa kuwa yanakinzana na suala la utunzaji wa mazingira kwa kuwa yatazuia upandaji wa miti inayokua zaidi ya futi tatu, ambayo kimsingi husaidia kutunza mazingira.

Mheshimiwa Spika, Aidha Kamati imebaini masharti yasiyo na uhalisia katika utekelezaji wake ni **Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe, 2019**

zilizotungwa chini ya **Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa (Sura 290)**. Jedwali la Kwanza linaweka sharti la malipo ya ushuru wa shilingi 100,000/- kwa gari lenye ujazo wowote wa mizigo ya mazao, au bidhaa mbalimbali kushusha mizigo na mifugo katika Masoko ya maeneo ya vivuko.

Mheshimiwa Spika, Sharti hili halina uhalisia kwa kuwa halizingatii ukweli kwamba magari ya kupakia mizigo yana uzito tofauti, hivyo hata ujazo wa mizigo unatofautiana kati ya gari moja na nyingine.

3.0 UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA KATIKA MKUTANO WA KUMI NA TISA WA BUNGE

Mnamo tarehe 8 Aprili, 2020 Serikali iliwasilisha Mezani nakala za Magazeti ya Serikali na viambatisho vyake zikiwemo jumla ya Sheria Ndogo Mia Moja Themanini na Nane (188) kwa mujibu wa Kifungu cha 38(1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura 1 na Kanuni ya 37(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Sheria Ndogo hizo zimegawanyika katika makundi yafuatayo:-

- a) Sheria Ndogo za Halmashauri (*By-Laws*) – 15;
- b) Kanuni za Wizara (*Regulations*) – 33;
- c) Amri (*Orders*) – 47;
- d) Matangazo (*Notices*) – 88;
- e) Kanuni za Taasisi (*Rules*) – 4; na
- f) Hati (*Instrument*) – 1.

Mheshimiwa Spika, katika mchanganuo wa Sheria Ndogo ulioainishwa, Kamati ilichambua na kubaini dosari mbalimbali katika Sheria Ndogo Sita (6) zilizo chini ya Wizara zifuatazo:-

- a) Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano;
- b) Wizara ya Katiba na Sheria; na
- c) Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, baada ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo hizo, Kamati imetoa maoni na ushauri kwa lengo la kuboresha

maudhui ya Kanuni hizo kama inavyoonekana katika **JEDWALI LA UCHAMBUZI** lililoambatishwa katika Taarifa hii. Kwa minajili ya kulitaarifu Bunge lako tukufu kuhusu uchambuzi uliofanyika, baadhi ya dosari zilizobainika katika Kanuni hizo ni kama ifuatavyo:-

a) **Sheria Ndogo kwenda kinyume na Sheria Mama au Sheria nyingine za Nchi.**

Mheshimiwa Spika, Katika Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge, Kamati imebaini baadhi ya Sheria zina masharti yaliyo kinyume na yale yaliyowekwa na Sheria Mama au na Sheria Nyingine za Nchi.

Dosari hiyo imebainika katika Kanuni za *The Natural Wealth and Resources Permanent Sovereignty) (Code of Conduct for Investors in Natural Wealth and Resources) Regulations, 2020* zilizotungwa chini ya Sheria ya *The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, (Sura 449)*. Kanuni ya **10** imeainisha makatazo tisa ya ubaguzi dhidi ya mwajiriwa ambayo kimsingi ni machache ikilinganishwa na makatazo ambayo yameainishwa katika kifungu cha 7(4) cha **Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura 366** ambacho kimeainisha makatazo kumi na tano ya ubaguzi dhidi ya mwajiriwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona ni vema Sheria Ndogo zinapotungwa zizingatie masharti ambayo tayari yamewekwa na Sheria Mama na au Sheria Nyingine za Nchi ili kuepuka kukinzana kwa Sheria ambapo ni kinyume na Kifungu cha 36(1) cha Sheria ya Tafsiri za Sheria, Sura 1.

b) **Sheria Ndogo kutozingatia misingi bora ya uandishi wa Sheria (drafting principles)**

Mheshimiwa Spika, Sheria Ndogo nyingine iliyobainika kuweka masharti yasiyo na uhalisia ni *The Electronic and Postal Communications (Sim Card Registration) Regulations, 2020* ambayo imetungwa chini ya *The Electronic and Postal Communications Act, (Sura. 306)*.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa kwa namna ambavyo imeandikwa inazuia umiliki wa laini ya simu zaidi ya moja kutoka katika Kampuni moja ya simu. **Kanuni ya 18 (1)** imeweka masharti ya idadi ya kadi za simu zinazopaswa kumilikiwa na mtu, Kampuni au Taasisi, ambapo kwa mtu binafsi hatapaswa kumiliki zaidi ya laini ya simu (*Sim Card*) moja (1) kutoka Kampuni mmoja ya simu kwa matumizi ya huduma ya kupiga, ujumbe mfupi wa maneno na matumizi ya mtandao (*Data*); na iwapo ni Kampuni au Taasisi, basi hazitapaswa kumiliki zaidi ya kadi ya simu thelathini (30) kutoka katika Kampuni moja ya simu kwa matumizi ya huduma ya kupiga, ujumbe mfupi wa maneno na matumizi ya mtandao (*Data*).

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kuwa ni vema uandishi wa Kanuni hii ukaonesha kuwa haiweki katazo la umiliki wa laini nyingi za simu kwa kadiri mtu, Kampuni au Taasisi itaona inafaa kufanya hivyo.

Aidha, inapendekezwa kuwa **Kanuni ya 18(3)** inayotoa fursa ya kuwasilisha maombi kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ya kumiliki laini za ziada tofauti na ilivyoainishwa kwa mujibu wa Kanuni hizi ifanyiwe marekebisho ili iainishe utaratibu wa namna ya kuwasilisha maombi ya laini za ziada kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania pamoja na utartibu wa kuzingatia iwapo mwombaji hataridhika na uamuzi wa mamlaka hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri ni vema katika siku za usoni sharti la kuweka idadi ya umiliki wa laini za simu likaondolewa, kwa kuwa wamiliki wa laini hizo za simu watakuwa wamezingatia taratibu zote za usajili. Badala yake Wizara na vyombo husika zitumie mifumo iliyopo kudhibiti namna bora ya matumizi ya laini hizo za simu zinazotumika pasipo kuweka ukomo wa idadi ya laini zinazopaswa kumilikiwa na mtu, kampuni au taasisi. Hatua hii itawezesha kupanua wigo wa makampuni kupata mapato mengi yatokanayo na kuwa na wateja wengi wanaotumia huduma zake, vilevile kutanua wigo wa Serikali kukusanya zaidi

mapato ya kodi mbalimbali zitokanazo na matumizi ya mitandao ya simu.

c) Sheria Ndogo kutoendana na uhalisia wa mambo ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini pia baadhi ya Kanuni za Wizara zimeweka masharti yasiyo na uhalisia na ambayo yanaweza kuleta madhara katika utekelezaji wake. Kanuni hizo ni *The Transport Licensing (Public Service Vehicles) Regulations, 2020* ambazo zimetungwa chini ya **Sheria ya The Transport Licensing Act (Sura 317)**, ambapo **Kanuni ya 26** inaweka sharti kwa mwenye leseni ya kutoa huduma ya usafiri wa mabasi ya shule kuwa na dereva mwenye umri usiopungua miaka thelathini na tano na miaka isiyozidi miaka sitini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kwamba, sharti la umri uliowekwa kwa mujibu wa kanuni halina uhalisia, kwa kuwa udereva hauzingatii umri tu ulioainishwa bali hutegemea uzoefu wa dereva husika katika kuendesha vyombo vya usafiri. Hivyo Kamati inashauri Kanuni iboreshwe kwa kuongeza sharti la kumtaka dereva mwenye leseni ya daraja la kuendesha mabasi ya shule awe pia na uzoefu wa kuendesha magari ya shule usiopungua miaka kumi.

d) Sheria Ndogo kukiuka misingi ya haki za binadamu

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwepo kwa Sheria Ndogo zinazokwenda kinyume na haki za binadamu. Sheria Ndogo hizo ni pamoja na *The Transport Licensing (Public Service Vehicles) Regulations, 2020* iliyotungwa chini ya Sheria ya *The Transport Licensing Act (Sura 317)*. **Kanuni ya 28(4)** inatoa fursa kwa mamlaka kusitisha leseni ya mtoa huduma ya usafirishaji pasipo kutoa fursa ya kumsikiliza mwenye leseni.

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kwamba, maudhui ya Kanuni hii ni kinyume na misingi ya haki za asili ambazo zinaweka sharti la mtu kusikilizwa kabla ya kupewa adhabu.

Hivyo Kamati inaona ni vema Kanuni zikaweka bayana mienendo na matukio yanayoweza kupelekea usitishwaji wa leseni pasipo kumsikiliza mtoa huduma. Hii itasaidia kuondoa uwezekano wa matumizi mabaya ya kanuni hii na kupelekea kusitishwa ghafla kwa huduma ya usafiri, kuleta usumbufu kwa watumiaji wa huduma ya usafiri husika pamoja na kuleta athari mbalimbali zitokanazo na uwekezaji uliofanyika katika huduma husika.

e) **Sheria Ndogo kuwa na makosa ya uandishi katika Majedwali (Kutorejea Kanuni sahihi, kurejea Kanuni ambazo hazipo, kutorejea kabisa Kanuni na Maudhui ya Jedwali kutofautiana na Vifungu)**

Mheshimiwa Spika, Kamati pia imebaini kasoro mbalimbali katika Majedwali yaliyopo katika Sheria Ndogo. Kasoro hizo zimebainika katika Sheria Ndogo ya *The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Regulations, 2020* iliyotungwa chini ya Sheria ya *The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act, (Cap. 450)* ambapo Fomu yenye Namba NWR Form - N.3 iliyo katika Jedwali la Tatu ina makosa ya uandishi kwa kutumia maneno yasiyo na muktadha unaoendana na Kanuni hii, ambapo maneno "**General Assembly**" yametumika badala ya maneno "**National Assembly**" ambayo ndiyo yaliyokusudiwa katika Fomu hii.

Mheshimiwa Spika, Sheria Ndogo nyingine iliyobainika kuwa na makosa katika Majedwali ni *The Transport Licensing (Public Service Vehicles) Regulations, 2020* iliyotungwa chini ya Sheria ya *The Transport Licensing Act (Sura.317)*. Katika Sheria hii ilibainika kuwa, Jedwali la Nne linaloonesha mfano wa orodha ya abiria wanaosafiri (*manifest*) limerejea kimakosa kuanzishwa chini ya **Kanuni ya 34** ambayo kimsingi inazungumzia haki ya mmiliki wa leseni kutoza nauli iliyoidhinishwa na mamlaka. Kamati iliona kuwa Kanuni sahihi inayoendana na maudhui ya Jedwali la Nne ni **Kanuni ya 33 (1)**.

4.0 MAPENDEKEZO YA JUMLA

a) Uandishi wa Sheria Ndogo

Kamati inashauri Mamlaka zilizokasimiwa jukumu la utungaji wa Sheria Ndogo, kuepuka kutunga Sheria Ndogo zinazoweka masharti ya jumla katika baadhi ya vifungu na badala yake, zitunge Sheria Ndogo zinazoweka vifungu vinavyofafanua kwa kina namna ya utekelezaji wa masharti mbalimbali yaliyowekwa na Sheria Mama.

b) Utoaji wa Elimu kuhusu masuala ya Sheria Ndogo na Ushirikishwaji wa Wadau

Kamati inashauri kuwa ni vema Wizara zikaendelea na programu za utoaji wa elimu kwa umma na kushirikisha wadau kwa karibu pale inapotokea kuna utungwaji wa Sheria Ndogo mpya zinazolenga kuweka utaratibu wa namna ya kusimamia sekta fulani. Ushirikishwaji kwa wadau wanaolengwa na Sheria Ndogo utapunguza changamoto mbalimbali zinazoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa Sheria Ndogo hizo.

Mfano kufuatia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kutunga Kanuni nyingi zinazohusu masuala ya usafiri wa barabara nchini, Kamati inashauri kuwa Wizara iandae programu za utoaji wa elimu kwa wamiliki wa vyombo vya usafiri, madereva, wafanyakazi na wananchi kwa ujumla ambao ni watumiaji wa vyombo vya usafiri, ili waweze kutambua haki na wajibu uliowekwa kwa mujibu wa sheria kuhusu masuala ya usafiri wa barabara.

c) Ushirikiano wa Taasisi/Wizara na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Kamati inazishauri Mamlaka zilizopewa jukumu la kutunga Sheria Ndogo kufanya kazi kwa karibu na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakati wa utungaji wa Sheria Ndogo, ili kupata ushauri mzuri wa namna bora ya uandishi wa Sheria Ndogo.

d) Mamlaka kutotekeleza maeneo ya Sheria mpaka pale ambapo marekebisho ya maeneo hayo yamefanyika

Kamati inashauri kuwa, Mamlaka mbalimbali ambazo Sheria Ndogo zake zimebainika kuwa na vifungu vyenye dosari mbalimbali, kusitisha utekelezaji wa vifungu hivyo hadi hapo mabadiliko yatakapofanyika kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati. Hii itasaidia kuondoa athari mbalimbali zinazoweza kutokea kwa wanaoguswa na Sheria hizo kutokana na utekelezwaji wake.

e) Kufanya marekebisho katika Sheria Ndogo zilizobainika kuwa na Dosari

Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kuzifanyia marekebisho Sheria Ndogo zote zenye dosari. Baada ya marekebisho hayo kufanyika na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali, Sheria Ndogo hizo ziwasilishwe Bungeni kwa mujibu wa Sheria.

5.0 HOJA

a) Sheria Ndogo kukinzana na masharti ya Sheria Mama au Sheria nyingine za nchi.

KWA KUWA, baadhi ya Sheria Ndogo zilizofanyiwa uchambuzi na Kamati zilibainika kuwa na vifungu vinavyokinza na masharti ya Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi.

NA KWA KUWA, kukinzana huko ni kwenda Kinyume na masharti ya Kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinachotoa sharti kwa Sheria Ndogo kutokwenda kinyume na masharti ya Sheria Mama.

NA KWA KUWA, kukinzana huko kunaifanya Kanuni husika kuwa ni batili kwa kiwango ilichokinzana.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Wizara zinazohusika, zifanye marekebisho katika Sheria Ndogo hizo ili kuondoa vifungu vinavyokwenda kinyume na masharti ya Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi.

b) Sheria Ndogo kuwa na dosari ya Uandishi wa Majedwali ikilinganishwa na Vifungu vya Sheria

KWA KUWA, katika uchambuzi wa Kamati imebainika kuwa baadhi ya Sheria Ndogo zina dosari mbalimbali katika majedwali kuhusu vifungu vinavyoanzisha majedwali husika.

NA KWA KUWA, kwa mujibu wa Kifungu cha 25 (2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinabainisha kwamba Majedwali ni sehemu ya Sheria.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Wizara ambazo Sheria Ndogo zake zimebainika kuwa na dosari katika Majedwali zifanyiwe marekebicho ili kuondoa dosari hizo.

c) Sheria Ndogo kutozingatia Misingi ya Uandishi wa Sheria (Drafting Principles)

KWA KUWA, katika uchambuzi wa Kamati imebainika kwamba baadhi ya Sheria Ndogo zina dosari mbalimbali za kiuandishi;

NA KWA KUWA, dosari hizo zimesababisha mantiki na madhumuni yaliyokusudiwa katika vifungu husika kutofikiwa na hivyo kuleta changamoto katika utekelezaji wake;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Wizara ambazo Sheria Ndogo zake zimebainika kuwa na dosari za kiuandishi zifanye marekebicho ili kuondoa dosari hizo.

d) Sheria Ndogo kutozingatia masharti ya Haki za Binadamu

KWA KUWA, uchambuzi wa Kamati umebaini uwepo wa Sheria Ndogo zenye vifungu vinavyokiuka misingi ya haki za binadamu;

NA KWA KUWA, utekelezaji wa vifungu hivyo unaweza kupelekea kukosekana kwa haki za msingi kwa walengwa wa Sheria husika

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Wizara ambazo Sheria Ndogo zake zimebainika kuwa na dosari katika vifungu vinavyokiuka misingi ya haki za binadamu zifanye marekebisho ili kuondoa dosari hizo.

e) Sheria Ndogo kuweka masharti yasiyo na uhalisia ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake, hali ya uchumi wa walengwa na viwango vya adhabu na faini

KWA KUWA, katika uchambuzi wa Kamati imebainika kuwepo kwa dosari zinazoweka vifungu vyenye masharti yasiyo na uhalisia;

NA KWA KUWA, dosari hizo zinaweza kupelekea kuwepo ugumu katika utekelezaji wake na hivyo kukandamiza wanaolengwa na Sheria Ndogo husika;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Wizara ambazo Sheria Ndogo zake zimebainika kuwa na dosari katika vifungu vyenye masharti yasio na uhalisia zifanye marekebisho ili kuondoa dosari hizo.

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na Bunge lako tukufu kwa kuweka utaratibu wa Taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuwasilishwa katika Bunge lako tukufu. Ni matumaini yangu kwamba utaratibu huu utakuwa endelevu na hivyo kuchangia katika maendeleo ya nchi yetu kwa kuwa masuala mengi yanayoibuliwa kutokana na uchambuzi wa Sheria Ndogo kwa kiasi kikubwa yanagusa maisha ya kila siku ya wananchi wengi.

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba nimshukuru Mhe. Jenista Mhagama (MB) – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu) kwa kuendelea kuweka uratibu mzuri ambao uliwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa kipindi chote cha Bunge la Kumi na Moja.

Aidha, niwashukuru Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, pamoja na watendaji wa taasisi zilizo chini ya Wizara husika waliofika mbele ya Kamati katika Bunge hili la Kumi na Moja na kujibu hoja zilizoibuliwa na Kamati. Kupitia majadiliano yenye tija katika vikao hivyo, imepelekea kufanyika marekebisho mbalimbali katika Sheria Ndogo zilizobainika kuwa na dosari.

Mheshimiwa Spika, vilevile kipekee kabisa nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mikutano iliyotangulia ya Bunge la Kumi na Moja pamoja na kuchambua Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Nane na Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge na hatimaye kuandaa Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Ni ukweli usiopingika kuwa kazi ya uchambuzi wa Sheria Ndogo ni ngumu kwa kuwa Sheria zinazowasilishwa Bungeni huwa ni nyingi, lakini pasipo kuangalia hilo Wajumbe wa Kamati hii wameifanya kazi hii kwa moyo na juhudi ya hali ya juu na hatimaye kuweza kuchambua Sheria Ndogo zote zilizowasilishwa katika Bunge la Kumi na Moja.

Kwa heshima kubwa naomba majina yao yaingie katika kumbukumbu rasmi za Bunge (*Hansard*):-

- i. Mhe. Andrew John Chenge, Mb - **Mwenyekiti**
- ii. Mhe. William Mganga Ngeleja, Mb - **Makamu Mwenyekiti**
- iii. Mhe. Aida Joseph Khenani, Mb
- iv. Mhe. Khamis Mtumwa Ali, Mb
- v. Mhe. Rashid Ali Abdallah, Mb
- vi. Mhe. Mlinga Goodluck Asaph, Mb
- vii. Mhe. John John Mnyika, Mb
- viii. Mhe. Halima James Mdee, Mb
- ix. Mhe. Elibariki Emmanuel Kingu, Mb
- x. Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mb
- xi. Mhe. Sabreena Hamza Sungura, Mb
- xii. Mhe. Sadifa Juma Khamis, Mb
- xiii. Mhe. Anne Kilango Malecela, Mb

- xiv. Mhe. Zainab Athman Katimba, Mb
- xv. Mhe. Salome Wycliffe Makamba, Mb
- xvi. Mhe. Twahir Awesu Mohammed, Mb
- xvii. Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb
- xviii. Mhe. Mary Deo Muro, Mb
- xix. Mhe. Easther Lukago Midimu, Mb
- xx. Mhe. Catherine Nyakao Ruge, Mb
- xxi. Mhe. January Yusuf Makamba, Mb

Mheshimiwa Spika, aidha napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Ndg. Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati hii ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, nimshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto akisaidiwa na Ndg. Gerald Magili, Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Kamati za Bunge kwa usimamizi mzuri wa Shughuli za Kamati.

Mwisho lakini si kwa umuhimu, niwashukuru Makatibu wa Kamati ya Sheria Ndogo Ndg. Angela Shekifu, Ndg. Stanslaus Kagisa, Ndg. Mkuta Masoli wakisaidiwa na Ndg. Paul Chima kwa kuratibu vyema Shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Andrew J. Chenge

MWENYEKITI

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO

5 Juni, 2020

SPIKA: Ahsante sana. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nakushukuru sana Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Ngeleja, kwa kutupitisha katika hoja.

Mwanzo kabisa, niwapongeze sana Wajumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa sana ambayo mmekuwa mkiifanya kuchambua sheria hizi nyingi,

voluminous lakini mmefanya kazi hiyo kwa uaminifu mkubwa na mmeishauri Serikali wakati kwa wakati kuhusiana na mambo yanayohusiana na sheria ndogo. Tunawapongeza sana na wakati mwingine pamoja na mzigo mlionao tuliwaongezea Miswada tena mingine na mlitusaidia kuchambua vizuri kabisa. Tunawashukuru sana kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya chini ya uongozi wa Mheshimiwa Chenge na Mheshimiwa Ngeleja. *(Makofi)*

Sasa tunaingia katika uchangiaji, ninayo baadhi ya majina hapa lakini Mheshimiwa ukijisikia kama una cha kusema siyo mbaya ukaniandikia ili niweke meza yangu vizuri. Ninazo nafasi kama mbili, tatu tu, chache sana lakini unaweza ukaniandikia ukiona yafaa kufanya hivyo.

Sasa basi tunakuja kwenye uchangiaji moja kwa moja, tuanze na Mheshimiwa Goodluck Mlinga, atafuatiwa na Mheshimiwa Salome Makamba. Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa ndiyo mwisho mwisho, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya na kuwa Rais ambaye anafanya maajabu kuliko Marais wote duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakumbuka mwaka 2017 tulipelekwa China kwa ufadhili wa Serikali ya China, tulikuwa Wabunge mchanganyiko, wa CCM pamoja na wa Upinzani. Kule wakakutana na msemu unaosema kuwa nchi ya China akipatikana Rais kama Dkt. Magufuli huwa wanabadilisha Katiba anakuwa Rais wa milele mpaka Mungu atakapoamua kumchukua. Tuliporudi nusu ya wale Wabunge wa Upinzani walihamia CCM wakiongozwa na Mheshimiwa Julius Kalanga.

Mheshimiwa Spika, mwanzo walisema huwezi kuiendesha nchi bila kusafiri kwenda nje lakini mpaka leo hii sijawahi kusikia wafanyakazi wakilalamika mishahara imechelewa na Rais hasafiri nje. Walisema huwezi kufanya

miradi mikubwa bila kusaifiri, nimeshuhudia *SGR* na *Standard Gauge* mpaka leo hii haijasimama inaendelea kwa kasi.

Mheshimiwa Spika, maajabu makubwa aliyoyafanya Mheshimiwa Rais, hii ndiyo alifunika ni kwenye vita dhidi ya Janga la Corona. Mheshimiwa Rais alisema hakuna *lockdown* wala baba yake *lockdown*. Tulishuhudia nchi kubwa zenye uwezo zikiweka *lockdown* lakini wagonjwa na vifo vilizidi. Tulishuhudia nchi ambazo zilitoa mishahara kwa wananchi wao wote yaani ziligawa fedha lakini wagonjwa na vifo vilizidi.

Mheshimiwa Spika, wapo majirani zetu ambao walikopa pesa kwa ajili ya vita dhidi ya Corona, Rais wetu alikataa, lakini zile fedha zimeisha na wagonjwa na vifo vinazidi. Kwa hiyo, napenda sana kumpongeza Mheshimiwa Rais kwenye hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia naomba nikupongeze wewe kwanza kwa kuianzisha hii Kamati yetu ya Sheria Ndogo. Katika mambo makubwa uliyoyafanya katika nchi hii, hili litaingia katika historia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kazi kubwa ambayo tunaifanya Wajumbe naomba tunapomaliza Bunge hili ungetuzawadia vyeti kwa sababu hii kazi tuliyofanya kuna Wabunge siyo wanasheria lakini wamekuwa wanasheria. Hata nchi za wenzetu huwa wanatoa vyeti kulingana na *experience* hata kama mtu hajaenda darasani. Kwa hiyo, hilo nalipendekeza pia.

Mheshimiwa Spika, naomba wanasheria ambao wanapewa mamlaka ya kutunga hizi kanuni wangukuwa makini kidogo kwa sababu makosa ni mengi mno kiasi kwamba madaktari wangewa wanafanya makosa kama haya Tanzania leo hii isingekuwa na watu. Kwa hiyo, naomba wanasheria ambao wamepewa mamlaka ya kutunga hizi sheria wasimamie vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuna sheria ambazo zinabagua wananchi wetu. Kwa mfano, hii Sheria ya Usafirishaji inasema

eti dereva ambaye anaendesha magari ya wanafunzi aanzie umri wa miaka 35. Kwa nchi zetu za Kiafrika miaka 35 mtu anakuwa ameshaanza kuzeeka. Hata katika Bunge lako Tukufu katika Mabunge yaliyopita kulikuwa na malalamiko mengi ambapo Wabunge walikuwa wanalala Bungeni mpaka wakawekewa pipi lakini hii sheria inasema eti mtu mwenye umri chini ya miaka 35 hawezi kuendesha magari ya wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, kwa mimi ninavyoamini mtu ambaye ana umri mkubwa na utendaji wa kazi za mikono uwezo wake huwa unapungua. Kwa hiyo, sheria kama hizi zilikuwa zinawabagua wananchi wetu na zinapingana na Katiba yetu ambayo inasema mtu kuanzia umri wa miaka 18 anatakiwa aweze kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, pia napendekeza hizi sheria kabla hazijaanza kufanya kazi ziwe zinaletwa Bungeni kwa sababu Wabunge ndiyo wawakilishi wa wananchi. Hizi sheria zinapoenda kufanya kazi kwa wananchi zinakuwa hazina mkono wa wananchi, matokeo yake zinakwenda kuwaathiri. Tumeona sheria nyingi sana zikiwakandamiza wananchi.

Mheshimiwa Spika, pia napendekeza sheria hizi kabla hazijaenda kutumika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ihusishwe. Kwa sababu tumeona sheria nyingi zinakwenda kutumika bila Mwanasheria Mkuu wa Serikali kushirikishwa matokeo yake kunakuwa na makosa mengi sana ya sheria. Kwa mfano, kukiuka Katiba na sheria mama; sheria ndogo nyingi sana zinakiuka sheria mama.

Mheshimiwa Spika, hayo yalikuwa mapendekezo yangu na naunga mkono hoja na nawapongeza sana Mwenyekiti wetu wa Kamati, Mheshimiwa Andrew Chenge na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Ngeleja kwa sababu wametulea vizuri hata sisi ambao hatukuwa makonki kwenye sheria sasa hivi tumekuwa makonki. Naamini huko mtaani tutakaporudi tutakuwa ma-*bush lawyers*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Goodluck Mlinga kwa kutuanzishia mjadala wetu. Nimeshamtaja Mheshimiwa Salome Makamba kwamba ndiye anayefuata na Mheshimiwa Mbaraka Dau ajiandae.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie kwenye Kamati hii ya Sheria Ndogo, Kamati ambayo nimehudumu kwa miaka yote ambayo nimekuwa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda nianze kwa kusema pamoja na kwamba Bunge letu ni moja kati ya Mabunge ambayo yanafuata utaratibu wa Nchi za Jumuiya ya Madola lakini kwa uzoefu nilioupata kwa kukaa kwenye Kamati hii ya Sheria Ndogo kwa muda mrefu nimegundua kwamba ile tulivyokasimu mamlaka ya kutunga sheria; Bunge limekasimu kwa mamlaka mbalimbali kwa Mawaziri, Halmashauri mbalimbali na taasisi mbalimbali za Serikali, kitendo cha kukasimu halafu wao wakishatunga zile sheria ndogo wakizileta hapa Bungeni baada tu ya kuzi-*table* sheria hizi zinaanza kutumika ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia mapungufu makubwa ambayo tumeyabaini kwa miaka mitano ambayo mengi ni mapungufu yanayofanywa kwa uzembe au kwa kutokufuata sheria na mengine yanavunja Katiba na mengine yanavunja haki za binadamu, ipo haja ya kuangalia upya zoezi la utungaji wa sheria ambalo tumelikasimu kwenye mamlaka mbalimbali ili zinapoletwa hapa Bungeni tuzipitie kwanza kabla hazijaanza kufanya kazi. Sheria ambazo tunazipitia wakati huo zimeshaanza kufanya kazi huko mitaani zinaleta madhara makubwa sana kwenye jamii, biashara na uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakutolea mifano michache hata kwenye hotuba yetu imeelezwa ambayo inasababishwa na sheria hizi ndogo ambazo kimsingi zimeshaanza kutumika pamoja na kwamba leo tunazijadili hapa Bungeni. Kuna Kanuni ambayo imetungwa na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kupitia Kanuni ya *Transport*

Licensing, Public Services Vehicle Regulation ya mwaka 2020. Kanuni hii inaweka sharti kwenye kifungu cha 18(1),(2) na (3) kwamba mtu mmoja anatakiwa kumiliki *line* moja ya simu kutoka kwenye mtandao mmoja na kama ni kampuni mwisho wake kumiliki ni *line* 30. Sasa hapa karibuni ililetwa biashara ya *NIDA*, vitambulisho tukasajili wakasema tumeweka alama za vidole, wanaweza kutu-*track* mpaka kijiji na mtaa na nyumba ninayokaa na mtendaji wangu wa mtaa. Kama nimesajili hii *justification* anayoileta Mheshimiwa Waziri kwamba wanajaribu kuzuia uhalifu kwa kuhakikisha mtu mmoja anamiliki *line* moja ya simu inatokana na msingi upi?

Mheshimiwa Spika, kampuni inaweza ikaamua inunue *line* nyingi kwa ajili ya wafanyakazi wake, unapoi-*limit* kampuni kwamba mwisho *line* 30 wakitaka kuongeza *line* wafanye maombi maalum. Haya mambo ya *telecommunication*, biashara za mitandao ya simu na line za simu faida ni ndani ya dakika moja na hasara ni ndani ya dakika moja. Unapom-*subject* mtu aende akasajili *line* ya simu aombe *TCRA* maombi yake yatachukua sijui siku saba au siku ngapi, tunataka kulifanya hili taifa la namna gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi sasa hii sheria imeshaanza kufanya kazi *as we speak*. Bunge hili limekasimu mamlaka na sheria imeanza kufanya kazi, nini *essence* ya kuwa na viambulisho vya *NIDA*, ni kwa nini tulikuwa tunasajili au tunataka kuonesha kwamba mfumo wa *NIDA* haufanyi kazi? Hiyo ndiyo tafsiri ambayo ninaipata kwenye kanuni hii. Kwa hiyo, kukasimu haya mamlaka Mawaziri wanakimbilia kwenda kujificha kwenye kanuni au mamlaka zinajificha kwenye kanuni wanatunga sheria mbaya.

Mheshimiwa Spika, kwenye sheria ya *Transport Licensing Public Services and Vehicles*, wameweka sharti kwa mtu anayemiliki vyombo vya usafirishaji...

SPIKA: Labda kidogo tu, Waheshimiwa mnaochangia leo kila mmoja ana dakika 15, kwa hiyo uhuru ni wako.

WABUNGE FULANI: Sawa.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwenye Sheria ya Usafirishaji wametengeneza kanuni, kwenye kanuni ile wameweka vifungu, Waziri anasema anao uwezo wa kumsitishia leseni msafirishaji anayefanya usafirishaji kwa njia ya mabasi au vyombo mbalimbali vya usafiri vya umma, ana uwezo wa kumsitishia kibali au leseni ya usafirishaji bila kumpa haki ya kumueleza wala kutoa sababu ya kwa nini anafanya hivyo na baada ya hapo hawaoneshi kama yule mtu hakuridhika na mchakato mzima wa kusitishiwa leseni anaweza kwenda kulalamika wapi, hawaoneshi, imekaa kimya. Sheria hii iko mtaani inafanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wanaenda mbali zaidi wanasema wamiliki wa mabasi wanatakiwa kutunza tiketi, zile tiketi walizotukatia, rekodi ya zile tiketi wanatakiwa wazitunze kwa miaka mitano. Hivi, kwa hizi *frame* ambazo tumejengewa hizi, miaka mitano, hizo tiketi utaziweka wapi? Wadau wenyewe wanakuja kwenye kamati wanalalamika. Wanasema hayo makaratasi ya miaka mitano mimi siwezi kuyatunza, Wizara ije ichukue ikaenayo.

Mheshimiwa Spika, sasa ndio haya tunasema wanatunga sheria ambazo hazina uhalisia, wanatunga sheria ambazo zinakwamisha biashara na hali ya uchumi kwenye nchi, wakati huohuo tunajinasibu kwamba, sisi ni nchi ambayo tunaenda kwenye Serikali ya viwanda, tunasema sisi tunawawezesha watu wanyonge, tunataka tuwawezeshe wafanyabiashara. Hizi *barriers* ambazo tunaziweka kwenye uwekezaji na biashara zinaleta ugumu mkubwa katika utendaji katika aneo la biashara.

Mheshimiwa Spika, kwahiyo mimi nikuombe, kabisa, kwa dhamira ya dhati; hizi sheria zisiishie kuwa *tabled* hapa Bungeni. Zikishakuwa *tabled* Bungeni zisifanye kazi mpaka sheria hizi zitakapokuwa zimepitiwea kwenye kamati ambayo tumeanzisha kwenye Bunge hili na zikipitiwa zidhibitike ndipo ziende zikafanye kazi mtaani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna sheria moja; amesema vizuri Makamu Mwenyekiti wangu wa Kamati; iko Buhigwe huko, ni Chato sijui wapi. Hiyo sheria wameweka masharti wanasema kila lori ambalo limebeba mazao litatozwa ushuru wa shilingi laki moja. Sasa, juzi hapa tulitoka kuambiwa lori lenye uzito chini ya tani moja lililobeba mazao litapita bure, sasahivi kila lori shilingi laki moja, sheria inafanya kazi, iko kule inafanya kazi inaumiza wakulima, inaumiza wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, nikuombe kwa moyo wa dhati hizi sheria zisifanye kazi. zipo sheria ambazo unakuta sheria moja, kwa sababu ya muda sitaenda ku-*refeer*. Sheria moja ina majedwali sita, majedwali yote yamekosewa yote sita, lakini kwenye Halmashauri kuna mtumishi ambaye analipwa mshahara kwa ajili ya utunzi wa hizi sheria, kwenye Halmashauri kuna kamati ambazo zinafanya kazi hii.

Mheshimiwa Spika, naendelea kusisitiza Bunge lijalo, niwepo au nisiwepo, Kamati ya Sheria Ndogo ifanye kazi ya kufanya *scrutinsation* ya hizi sheria kabla sheria hizi hazijaenda kwa Wananchi. Ninafahamu kwamba, tulikuwa tuna lengo la kupunguza mzungu mkubwa wa utungaji wa sheria kwa Bunge na ndiyo maana tukakasimu mamlaka haya. Hata hivyo nikuhakikishie zaidi ya asilimia 65 ya Sheria Ndogo ambazo zinatungwa zina mapungufu. Mapungufu yale ni makubwa kwa kiwango ambacho yanasababisha madhara makubwa kwenye jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimekumbuka kuna sheria moja iliwahi kutungwa ililetwa kwenye kamati yetu, iko Tabora, Halmashauri ina-*refeet* Ziwa Nyasa. Sasa sheria ni ya Halmashauri ya Tabora, *reference* iko Ziwa Nyasa, wana-*copy* na ku-*paste*, sheria ya eneo moja inawekwa eneo jingine. Kwahiyu ili kutibu haya ni lazima tuzingatie hilo.

Mheshimiwa Spika, mimi niende moja kwa moja kwenye sheria hii ya usafirishaji. Waziri ametunga kanuni, anasema hizi gari za kusafirisha wanafunzi, ya shule dereva anatakiwa awe na umri usiopungua miaka 35 mpaka miaka 60. Sasa, Katiba yetu iko wazi, mtu anaruhusiwa kufanya kazi

akiwa na umri wa miaka 18, anaruhusiwa kufanya kazi. Naelewa *concern* ya Wizara, kwamba wanataka kuweka watu angalao kidogo wenye *maturity* na wenye umakini ili waweze kuwaendesha watoto wetu. Lakini, kwa mfano unaweza kuwa na miaka 35 ukiwa umeanza kuendesha gari ukiwa na miaka 32, hiyo haimaanishi kwamba, wewe ni dereva mzuri barabarani. Unaweza kuwa na umri wa miaka 55 kumbe umekuwa *declared* kwamba, hauwezi kuendesha gari hauoni vizuri.

Mheshimiwa Spika, ka hiyo, ushirikishwaji wa wadau katika utungaji wa hizi sheria ni jambo ambalo Wizara na Serikali haiwezi kullepuka, wawashirikishe wadau, ili kuweza kujua *requirement* ni nini. Changamoto ipo nakubaliana kwamba, watoto wetu wanahitaji watu makini.

Mheshimiwa Spika, tumewashauri vizuri kwenye Kamati, hawa watu wanaomiliki mabasi ya shule kwenye basi la shule kuwe kuna *nurse*, yule msaidizi ambaye anaangalia wale watoto ili dereva afanye kazi yake ya kuendesha na yule msaidizi atusaidie katika kuwashusha watoto na kuwavusha barabara na si kuweka kigezo cha umri kama ndiyo busara au hekima kubwa ya mtu anayeweza kuwaendesha watoto wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nashauri umri wa dereva anayeendesha mabasi ya shule urudi kuwa miaka 18, lakini umakini mkubwa katika kufanya *interview* ya madereva wanaoendesha hayo magari uwepo, ufanyike. Ifanyike *due delegece* ili kuweza kujua uwezo wa...

SPIKA: Mheshimiwa Salome, ile nia njema iliyo ndani ya jambo hilo wewe huioni?

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, nimesema kwamba, mtu anaweza kuwa na miaka 18 na akawa dereva mzuri sana, na mtu anaweza akawa na miaka 55 akawa dereva mbaya. Kwa hiyo umri si busara au umri si umakini, kikubwa wapime uwezo wa dereva...

SPIKA: Huoni sio rahisi kumpata dereva wa bodaboda wa miaka 40 anayekwenda hovyohovy kama hawa vijana wa miaka 18, huoni ni...

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, umetoa mfano mzuri sana. Kumbe kuna madereva wa bodaboda wana miaka 40 na bado hawaendeshi vizuri...

SPIKA: Hayupo wa miaka 40 hamna.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: ...na vivyo hivyo kunaweza kuwa kuna madereva wa magari wenye *Class C*, ana miaka 40 na hawezi kuendesha gari kwa umakini mkubwa kuwalinda watoto wetu. Kwahiyo kigezo cha umri mimi sioni kama ni kigezo halali cha kumuweka mtu kuwa dereva wa gari za wanafunzi. Waangalie weledi, uzoefu, historia ya dereva na mambo mengi ambayo yanatakiwa kuzingatiwa ukiacha suala la umri. Kwa sababu, hata kwa kufanya hivyo pia, unakiuka Katiba yetu ambayo tumei...

MHE. MANSOOR S. HIRAN: Mheshimiwa Spika, naomba taarifa.

SPIKA: Afadhali itoke Taarifa bwana. Mheshimiwa Mansour.

T A A R I F A

MHE. MANSOOR S. HIRAN: Mheshimiwa Spika, naomba nitoe taarifa kwa mzungumzaji anayezungumza, kwamba naomba suala la watoto wa shule tusilinganishe na wanaoendesha bodaboda. Suala la watoto wa shule kwa kweli, umri ni muhimu sana kuangalia, umri wa miaka 18 ni mdogo sana. Naomba nimpe Taarifa hiyo, asante. (*Makofi*)

SPIKA: Anachosema Mheshimiwa ni kwamba, kinachozungumzwa hapa sio umri wa mtu tu lakini vilevile uzoefu katika uendeshaji, lakini pia awe mtu mzima ambaye ana familia, ana nini, yaani siyo kijana fulani ambaye yeye ndio anaanza maisha hajali. Lengo ni kuwalinda watoto

wadogo kwa kweli. Kwasababu mahali popote pale inapotokea ajali kama ile iliyotokea Arusha, wale watoto walipokuwa wakielekea Ngorongoro. Vinapotokea vifo vya watoto ni jambo ambalo linawagusa sana watu. Hoja yako ninaiona na sio kama tunau-*quash* mchango wako, tunakujazilia tu.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, mimi labda nimwambie aliyenipa taarifa alikuwa anakupa wewe maana wewe ndiwe uliyeleta ajenda ya bodaboda hapa, mimi sijaongea mambo ya bodaboda. Kwahiyo niseme tu, kwamba hayo maneno unayoyasema ni mazuri sana; lakini wewe Mheshimiwa Spika, umekuwa unakuja kwenye Kamati yetu muda mrefu na mara kwa mara; hayako kwenye kanuni; hayo ya kusema familia, awe sijui na uzoefu. Humu wameandika anatakiwa awe na umri wa miaka 35 mpaka miaka 60, na hayo unayosema ndiyo tuliyoyashari kwenye Kamati. Kwamba badala ya kuweka umri ukaleta mgongano wa Kikatiba wewe andika tu awe na uzoefu, awe ana *Class C*, hayo unayosema sasa wewe Mheshimiwa Spika, na *factors* nyingine zizingiwe.

Mheshimiwa Spika, lakini ukiandika kwenye kanuni moja kwa moja ambayo leo inaingia kwenye Azimio la Bunge, kwamba umri wa dereva anayetakiwa kuendesha magari ya watoto anatakiwa awe na umri wa miaka 35 mpaka 60 unajaribu ku-*invite* tu wale wanaharakati wa vijana na mambo ya uvunjifu wa Katiba na mambo kama hayo. Kwa hiyo tusiya-*invite* kwenye kanuni zetu kwa kuweka tu wazi sifa za mtu anayetakiwa kuendesha magari ya wanafunzi, mimi nadhani hapo tutakuwa tumeiweka vizuri.

Mheshimiwa Spika, basi baada ya kusema hayo...

SPIKA: Mimi nakubaliananawe, lakini nikuhakikishie hujaelewa tu ile *gist* ya Wizara. Waiweke kiuandishi kama unavyoshauri, lakini ile *gist* ya Wizara ni kuweka usalama zaidi kwa watoto wetu kwa kweli. Hata kama wewe una mtoto wako halafu una gari nyumbani unampa kijana wa miaka 18 awe anakupelekea shule na kurudi ni wewe *you can do*

that lakini kama kuna *alternative* utampa mtu mzima zaidi mwenye uzoefu, n.k., lakini sasa waiweke katika hiyo unayosema.

Yani tunakubaliana kimsingi, lakini kwamba kijana wa miaka 18. Maana yake ameanza kuendesha juzi *any how*, sasa huwezi kujifunzia kwa watoto wadogo ni hatari, tunajaribu kuwalinda watoto, si tuna Sheria ya Watoto pia?. Tunakubaliana na wewe, hatubishani, lakini kuliweka tu vizuri. Magari ya watoto yako mangapi Tanzania? Hata 200 hayafiki, sasa kwa nini haya machache haya yasiendeshwe na watu ambao ni wenye uzoefu zaidi.

Kwa hiyo Wizara nafikiri wamesikia wataliweka vizuri katika namna ya kisheria ya namna hiyo ambayo mnashauri, wala mimi sipingi lakini ni vizuri siku zote; ndiyo maana hata walimu wenyewe; wazuri sana wa chekechea na darasa la kwanza ni wale walimu wazee, watu wazima wale. Ndio wanakuwa walimu wazuri zaidi kuliko kijana mwalimu wa miaka 18 akawa ndiye mwalimu wa chekechea, unakuta kidogo haiendani. Watoto wadogo na babu zao wanaendana vizuri. Hiyo miaka 18 anaweza akaanza tena na ubakaji wa watoto, nini, shida tu, wana matatizo mengi sana Mheshimiwa Salome, hujaelewa tu.

Mheshimiwa Mbaraka Dau.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa fursa hii ili na mimi niweze kuchangia hoja hii ya Taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujaalia uzima na afya tumeweza kukutana hapa kwa ajili ya kujadili masuala yanayoihusu nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru sana wewe. Mimi ni Mbunge wa awamu ya kwanza, wanaita *form one*. Nilipokuwa ninawaulizauliza wazoefu hapa walisema kwamba, uwepo wa Kamati hii ya Sheria Ndogo ulikuwepo hata Bunge lililopita, lakini makali na meno yake hasa

yamekuja katika Bunge hili la kwako. Kwa kudhihirisha hivyo ukiipitia Taarifa ya Kamati, Kamati inasema imeshapitia Sheria Ndogo zaidi ya 2,601.

Mheshimiwa Spika, na miongoni mwa hizo Sheria Ndogo 2,601 sheria 547 zimefanyiwa marekebisho mbalimbali. Mwenye kufahamu ni Mwenyezi Mungu tu, kwamba ni kwa namna gani wananchi ambao pengine kutokana na uwepo au kasoro na dosari zilizojitokeza katika utungaji wa sheria hizo 547 ambazo Kamati yako Tukufu ya Sheria Ndogo imefanya marekebisho ya zile dosari kwa kweli, tunakushukuru sana kwa kuhakikisha kwamba, hili linafanyika ndani ya utawala wa kwako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 64 ya Katiba ya nchi yetu inatoa fursa na inalipa nguvu Bunge kuwa ndicho chombo ambacho kitakuwa kinawajibika na utungaji wa sheria zote za nchi hii zikiwemo hata hizo kanuni na *by laws* mbalimbali. Hata hivyo, sote humu ndani tunakubaliana kwamba kila kitu kikiletwa humu ndani kwa maana ya kanuni, kwa maana ya sheria na miongozo mbalimbali ikiletwa humu ndani, pengine Bunge hili litatakiwa lifanye kazi usiku na mchana kwa siku zote 365 na bado hatutaweza kuzipitia sheria zote. Na ndiyo maana basi Ibara ya 95(5) ikatoa mamlaka na kukasimu, kwamba Bunge lako sasa limekasimu madaraka katika mamlaka mbalimbali za chini ikiwemo Baraza la Madiwani, wakiwemo Mawaziri wanaotengeneza kanuni, ili kuweza kutusaidia kwa kuwa hatuwezi tukatunga sheria zote humu ndani zitakuwa ni nyingi sana. Sasa zile ndogondogo na zile kanuni mbalimbali Bunge lako limekasimu madaraka kwa mamlaka nyingine ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini inavyoelekea *practise* ni kwamba, labda huu mwanya wa kukasimu madaraka umekwenda kidogo umekuwa kama zile *delegated authorities* zimekuwa kidogo zina-*abuse* hii *privillage*. Na ndiyo maana ukaipa meno kamati yako hii ndogo, kwamba sasa zile sheria ndogondogo, kanuni, zinazotungwa na Mawaziri wenye dhamana na mamlaka nyingine huko chini zije zipitiwe sasa na Kamati yako Ndogo ya Sheria ambayo imetusaidia

kupunguza matatizo ambayo yanaonekana kule katika utekelezaji wa sheria mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yamesemwa mengi hapa kama mfano, na mimi nitaongeza kidogo mifano michache kwa mujibu wa taarifa hii ya Kamati yako ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano; Halmashauri ya Mkinga wanasema kwamba wametengeneza sheria ndogo, *by law* yao, kwamba mazao yanayozalishwa pale yakitaka kuhama kutoka kwenye Halmashauri kwenda Halmashauri nyingine kutakuwa na tozo ya asilimia tano. Sasa tayari kuna sheria inayosema, na Mheshimiwa Rais amekuwa akisisitiza tulishapunguza kwamba, itakuwa ni asilimia tatu, lakini Halmashauri huko imekaa imeweka asilimia tano. Unajikuta kwamba migongano kama hii sasa kupitia Kamati yako hii ya Sheria Ndogo ndiyo imeweza kuibaini na kuweka sawa mambo, ili wananchi kule waweze kunufaika na masuala mbalimbali yanayohusu maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa hapa suala la umiliki wa simu na ninaamini bado liko katika mapendekezo. Kwamba kwa *line* za simu ni mtandao mmoja kwa mtu mmoja. Inaonekana kwamba, labda pengine katika utungaji wake waliharakisha sana hawakuweka umakini na mapendekezo yamekuja kwamba, tubadilishe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu, kuna mtu mwingine ana *line* ya simu anatomia kwa *voice* na kutuma *massage*; lakini pia mimi naweza nikawa na *line tiGO* hiyohiyo ninaitumia labda kwenye *tablet* yangu na *line* ya *tiGO* hiyo naweza nikaitumia kwenye *device* nyingine. Kwasababu mwenyewe ninapenda labda *TTCL* kwamba *TTCL* ninaiona mtandao wake wa *data* ni rahisi na ni mpana zaidi. Kwahiyo sasa ukiniambia kwamba, niwe na *line* moja *in a way*ni kama vile unanibania uhuru wangu.

Mheshimiwa Spika, sasa hili nimeliona kama limekuwa bado lipo katika mapendekezo kuhakikisha wenzetu ambao wanahusika kule walirekebishe, ili mtu aweze kuwa na *line*

za simu mradi tu anafuata sheria na taratibu zilizowekwa na kwa kwa kuwa hivi sasa mambo yote yako ki-*digital* tunaweka alama za vidole sidhani kwamba kutakuwa na *abuse* ya aina yoyote. Tufungue hii mipaka, ili wananchi waweze kunufaika na haya masuala.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo hata mimi mwenyewe nimeli-*experience, fast hand* kabisa. Kule kwenye Halmashauri yangu, na hili jambo nimekuwa nikilizungumza sana mara nyingi bahati mbaya leo wenye dhamana siwaoni hapa, lakini kule Mafia ambako mimi ndio Halmashauri ninayoihudumia, imewekwa kanuni na Waziri wa Uvuvi na Mifugo, kwamba mtalii yeyote anayeingia katika maeneo ya hifadhi ya bahari anatakiwa alipe dola 24. Hiyo dola 24 ni kitendo cha yeye ku-*cross* ile *barrier* pale akaingia katika maeneo ya hifadhi. Masuala ya kulipia hoteli, chakula chake na mengine, hayo hayamo. Kila siku iendayo kwa Mungu; kwa maana nyingine akikaa siku tano, akikaa wiki moja, akikaa wiki mbili wanazidisha mara 24. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukasema jamani hii kanuni inatufanya tunakuwa *less competitive* kwenye utalii na utalii wa kwetu unakuwa na gharama kubwa. Na ukizingatia kwamba, *well*, hatu-*compete* na Zanzibar bali tuna-*complement each other*, lakini Zanzibar hiki kitu hakipo.

Mheshimiwa Spika, sasa mtalii anaona kwamba, kwa kitendo mimi cha ku-*step in* Mafia peke yake natakiwa nilipe dola 24, tena imekwenda mbali zaidi wanatoza mpaka kwa watoto, lakini kwa kiwango cha chini.

Sasa mtalii anakuja anasema hata ile *fees* yenyewe, ile *monetary value* yake siioni kwa sababu nakwenda ninakuta mazingira hayo yanayosemwa kwamba yamehifadhiwa wala hayako safi sana, wakati ule ma-*plastic bags* yameeneaenea kule pwani na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi katika eneo hili na nimeona Kamati mwisho huku imetoa ushauri...

SPIKA: Yaani Mheshimiwa Dau ni kwamba hata kama akiwa hotelini siku hiyo hakuingia baharini ni *24 dollars* au kila akienda ndiyo *24 dollars*?

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Spika, *no, no*. ipo hivi; ukishafika kiwanja cha ndege pale ukapanda gari, kuna maeneo yamewekwa yale maeneo yenye *beaches* nzuri yote ndiyo yanaitwa maeneo ya hifadhi, siyo baharini, hukuhuku nchi kavu. Kwa hiyo kuna *barrier*, ukifika kwenye *barrier* pale unajandikisha maana yake umeshaingia eneo la hifadhi ya bahari. Sasa *from that day* wewe utakuwa unalipa dola 24 kwa sababu kule ndiyo kwenye hoteli, huna namna ya kukimbia kwa sababu hoteli yako iko kule. Kwa hiyo ukilala kule, hata kama ukiamua umekaa hotelini tu unalala na kuamka ujue kwamba kuna tozo ya dola 24 *every day*.

Mheshimiwa Spika, sasa hili jambo tulikuwa tukilizungumza sana hapa na nilishamwomba na katika hotuba yake ya bajeti Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi aliahidi kwamba ataifanyia kazi kwa sababu inatuletea kidogo shida utalii unaonekana gharama yake ni kubwa Mafia ukilinganisha na maeneo mengine.

Kwa hiyo mimi kama Kamati ambavyo mwisho imetoa ushauri, nitaasisitiza baadaye, naliomba Bunge lako tukufu kupitia kwako, labda sijui pengine sisi wengine siyo wazoefu sana humu ndani, utengenezwe utaratibu ambapo kama Mbunge anaona kuna kanuni fulani, maana yake sheria ni jambo lingine, lakini kuna kanuni fulani, hususan katika maeneo ambayo tunahudumu kule kwenye halmashauri ina matatizo basi kuwe na kamwanya sijui ama kwa kwenda kwenye Kamati husika ya Sheria Ndogo ili kwenda kuli-*table* lile katika namna ambayo ni nzuri itakayotengenezwa na Bunge waweze kulipitisha. Nasema hivi kwa sababu Bunge lako na *Hansard* itakuwa ni shahidi, mimi kwa miaka yote minne na miezi kadhaa humu ndani hakuna hotuba ya bajeti ambayo sijazungumzia hilo jambo, lakini kumekuwa na ahadi tu kwamba tutalifanyia kazi, michakato inaendelea na vitu kama hivi.

Mheshimiwa Spika, sasa labda pengine tungekuwa na namna ya moja kwa moja sasa ya Mbunge kama vile ambavyo tunaweza kuwasilisha *private member motion*, basi na hii ya kurekebiha kanuni fulani kuwe na ka-*avenue* ili Mbunge sasa aweze kufanya hivyo tuweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la, kama Kamati ilivyofupisha...

SPIKA: Labda nikushauri Mheshimiwa Dau; kwa vile tuko katika kipindi cha kupitia kanuni kwa ajili ya Bunge lijalo, hebu pitia Kanuni zetu hizi angalia kama kuna mahali panapoweza ku-*fit* hili pendekezo, utuletee mapendekezo hayo haraka iwezekanavyo. (*Makofi*)

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na nakuahidi kwamba nitafanya hivyo ulivyoelekeza. Kwa bahati nzuri niko karibu sana na Mheshimiwa Mtemi Chenge ambaye ni gwiji wa sheria humu ndani. Nitakwenda kuomba pale ushauri kuangalia namna gani ya kutafuta ka-*avenue* ambacho naweza nikalipitisha hili jambo pengine ndani ya hizo wiki mbili zilizobakia basi liweze kufanikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niunge mkono tu ushauri ambao umetolewa na Kamati hii kwenye taarifa yake. Moja ya ushauri wamesema kuwe na utoaji wa elimu na naamini hilo ni jambo bora kabisa katika haya yote. Lazima kuwe na utoaji elimu, huko kwenye halmashauri huko kuna vurugu nyingi sana, watu hawajui.

Mheshimiwa Spika, binafsi tulikaa kwenye Baraza la Madiwani, kuna siku yakaletwa pale mapendekezo ya sheria ndogo (*by laws*), ikatengenezwa hoja pale wakasema tukimpata mwananchi anatupa takataka mtaani basi adhabu yake iwe Sh.50,000. Nikasema jamani inawezekana tunapenda maeneo yetu yawe masafi, tunapenda kulinda mazingira, lakini hii adhabu naiona kama ipo *over and above*. Tutengeneze mazingira tuweze kumbana ambaye anachafua mazingira, lakini kwa kweli kumwambia alipe Sh.

50,000 mtu wa kijijini tuta-*end up* na kuwafunga watu wengi sana kule vijijini.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka niongezee kwenye ushauri kwenye taarifa ya Kamati ni kwamba tumeona kuna tozo, majina ni mengi; tozo, ushuru, sijui vitu gani na Wizara zenye dhamana zimepewa mamlaka hii, Waziri anatengeneza hizo kanuni. Sasa nadhani labda kwa maeneo ambayo yanahusiana na utozaji wa...

SPIKA: Tayari dakika 15 ulishazitumia.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naunga mkono taarifa ya Kamati. (*Makofi*)

SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mbaraka Dau, Mbunge wa Mafia Kisiwani kule, tunakushukuru sana kwa mchango wako. Kwa kweli ulipotaja takwimu za kwamba mmepitia zaidi ya kanuni 500 katika *almost 2000 plus* zina matatizo nikajuliza sana, wenyewe wanasema *what is not happening*. Hata hivyo, moja ya vitu ambavyo unakutana navyo hasa kama umefanyafanya kazi halmashauri, nasi tumekuwa Madiwani wa halmashauri *for sometime*, sijui AG utafanyaje lakini ni *feeling* yetu sisi wengine kwamba kwa sasa hivi liko tatizo la *training* ya Wanasheria; tatizo kubwa sana.

Vyuo ni vingi sana, karibu kila chuo kinatoa wanasheria, hata hivyo vyuo tunavyoviaminia kama Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wanafunzi wake wengi sana, sijui siku hizi ni wangapi *batch* ya mwaka mmoja inayoingia, nafikiri labda 200 *plus*, sasa inakuwa si madarasa ni mikutano ya hadhara, kwa hiyo wanatoka watu ambao kwa kweli yaani kwenye halmashauri kule ni shida. Watu kule siku zote wanachukulia Mwanasheria ni msomi. Sasa Madiwani wa darasa la saba wanashangaa Mwanasheria huyo mweupe, yaani mweupe kabisa, wanawashangaa kweli. Kwa hiyo nadhani *there is something that has to be done somewhere* ili kuirudishia hii kada heshima yake na nafasi yake, vinginevyo liko tatizo *somewhere*, yaani acha kabisa.

Tunaendelea na anayefuata; Mheshimiwa Sakaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Lema. Kabla ya Mheshimiwa Sakaya, Waheshimiwa Wabunge mkishamwona Spika hana barakoa maana yake ni kwamba mambo *mswanu*. Kwa hiyo msihofu, siyo mbaya kuwa huru zaidi, kama hu-*feel like suffocating*. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Sakaya, tuendeleo.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi, pia nawapa pongezi sana Kamati hii ya Sheria Ndogo kwa kazi nzuri waliyofanya na kazi kubwa waliyofanya kuweza kuchambua sheria hizi na kutuletea mapendekezo hapa Bungeni tuyachangie na tuone namna ya kuweza kusaidia Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Waheshimiwa waliochangia wote kwamba kiukweli Bunge limekasimu mamlaka ya kutunga sheria ndogo kwenye maeneo mbalimbali huko chini, lakini bahati mbaya pia tumekasimu mamlaka kama Bunge lakini hatufuatilii kuona kilichotengenezwa kule ni kitu gani. Kwa hiyo matokeo yake tumekasimu mamlaka, tumeacha sheria zinatengenezwa, zinaanza kutumika mpaka tunakuja kugundua kwamba tayari zina madhaifu tayari watu walishaumia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi nakubaliana pia na mapendekezo kwamba tulipokasimu mamlaka yetu kama Bunge zinavyotengenezwa sheria ndogo popote, iwe ni kwenye Serikali za Mitaa kwa maana ya halmashauri zetu, kwenye manispaa, hata kwenye Wizara mbalimbali kabla ya kutumika liwepo jicho angalau la kuangalia ili kuhakikisha kwamba zile zilizotengenezwa kweli zina maudhui yaliyotarajiwa, lakini pia haziumizi wale ambao wanaenda kuzitumia hizo sheria.

Mheshimiwa Spika, tukifanya hivyo naona kama sasa hivi Kamati yetu hii ya Sheria Ndogo kwa muda huu wamepitia sheria nyingi na nina imani kabisa hawakuweza kupitia zote, wangeweza kupitia nyingi zaidi, lakini muda

hautoshi, kwa hiyo inawezekana kabisa kila sheria inayotungwa huku chini ina madhaifu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwa mfano sheria hizi za ushuru mbalimbali, kila halmashauri sasa hivi inajiwekea ushuru wake mwenyewe. Utakuta labda baadhi ya halmashauri moja inasema tenga moja la kuku Sh.2,000, halmashauri nyingine inasema tenga moja la kuku Sh.5,000, nyingine inasema tenga moja la kuku Sh.10,000, kila mmoja anajiwekea mwenyewe sasa *standards* ziko wapi? Kama tungekuwa tunafuatilia tungeweza kuweka *standard* kwamba kuendana na mazingira haya halmashauri hii angalau kiasi hiki ili kuhakikisha kwamba wafanyabiashara hawaumii, lakini pia wale wananchi wenyewe hawaumii. Kwa hiyo hilo ni mojawapo kwamba linaumiza watu.

Mheshimiwa Spika, pia kuna hii sheria ambayo tulibadilisha hapa Bungeni mwaka 2017, Sheria ya Ushuru wa *Cess* ya Tumbaku. Ilikuwa nchi nzima maeneo ambayo yanalima tumbaku *cess* ilikuwa ni Sh.5,000 na kwa bahati nzuri upande wa tumbaku *cess* ndiyo inasaidia sana halmashauri zetu kuweza kupata mapato ya kujiendesha kwa sababu mikoa inayolima tumbaku kwa mfano wilaya ambazo zinategemea tumbaku kama Kaliua, *cess* ndiyo inachangia pato kubwa sana katika mapato ya ndani.

Mheshimiwa Spika, tulivyobadilisha ile sheria hapa Bungeni 2017 tayari halmashauri zilikuwa zimeshaweka makisio yake kwenye bajeti, lakini pia bado zile hela kampuni ya tumbaku ilikuwa imeshatenga ile fedha kwa maana ya asilimia tano, lakini tulivyotamka hapa Bungeni tu kwamba ni asilimia tatu makampuni yale yakasitisha palepale, hayakutoa tena ile fedha na ile halmashauri kule tayari bajeti imeshaathirika. Kwa hiyo sasa unaona halmashauri nyingine bado ndiyo maana unaona leo wanasema kwamba baadhi ya halmashauri zimeendelea kutoa huo ushuru. Tayari zilikwa nayo kwenye bajeti zao, kwa hiyo baadhi ya mipango yao ilikuwa tayari imeshakwazika, ndiyo wengine wakasema angalau waendeleo kumalizia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo pia nashauri pale ambapo Serikali inataka kufanya mabadiliko kwenye sheria kuhusu ushuru mbalimbali wa halmashauri iangalie pia kule chini kabla ya kufanya huku juu. Kiukweli kama Halmashauri yetu ya Wilaya ya Kaliua tuliathirika sana na *cess* kipindi kile, lakini baadaye tumekuja ku-*cover* mpaka leo ile fedha ya mwaka mzima makampuni yanasema kwamba tulikuwa tumeshatenga lakini Serikali imebadilisha na kule halmashauri inasema tulikuwa tumeshaweka kwenye bajeti zetu tunaomba mtupe. Kwa hiyo kukawa na mgongano huo, tumefuatilia mpaka leo hawajaweza kutoa. Hata hivyo, ni ishara kwamba kuna ulazima sasa angalau kuweza kuwepo na *consensus* kabla ya kubalisha sheria za halmashauri ili kuhakikisha kwamba haziathiri halmashauri, lakini pia Serikali pia inaendelea kutimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie hili suala la umri kwenye sheria ya uendeshaji wa barabarani walilozungumzia Waheshimiwa Wabunge wenzangu na hasa suala la umri wa kuendesha magari ya shule. Mimi binafsi natamani kwamba magari ya watoto ya shule yaendeshwe na watu ambao kidogo wameshaona maisha, wameshakutana na *challenges* mbalimbali, wanaweza kuendesha angalau, saa nyingine unaona vijana wanavyopeleka wale watoto barabarani mpaka unaumia, unasema natamani angeendesha lakini ukiangalia angalau ule umri mkubwa wana kitu walichokuwa nacho, kwa sababu huyu mtu kuna kitu anachoona mbele zaidi. Kwa hiyo nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kwamba kigezo kisiwe ni umri, lakini kwenye mabasi ya shule tumeona tusirudi nyuma, kwenye mabasi ya shule lazima angalau kuwepo na *age* inayoonesha kwamba huyu mtu amekuwa *matured enough*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tunaona bodaboda barabarani, bodaboda mimi nalia tangu imeanzishwa kubeba abiria mpaka leo. Mtoto wa miaka 18 anapaa na bodaboda juu, mtu kama huyu ukimpeleka kwenye basi la watoto kesho atatuungiza kwenye shimo tu; haja-*mature*, hajui maisha, hana *commitment*, hajajiandaa chochote, ndiyo maana hajifunzi. Atakufa mwenzao hapo barabarani sasa hivi, watakusanyika

100 au 200 wakimaliza kuzika kichwani haipo; ni kwa sababu ya *mentality* zao, lakini kwa mtu ambaye ana umri mkubwa nina imani kabisa hata ikitokea tutasema kuna bahati mbaya hatukatai.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwenye sheria hii nikubaliane na Kamati kwamba umri usiwe ni kigezo pekee na vigezo vingine, *experience*, umakini, lakini kwa mabasi ya watoto ya shule tuwe na *standard* ya umri ambapo itaonekana kwamba huyu mtu yuko makini. *Otherwise* yaliyotokea Arusha yataendelea kutokea maeneo mengine, tutaendelea kupoteza watoto wetu, tuone kwamba hawa ni watoto ambao wana *future* zao, wana ndoto zao, mtu mmoja tu akishindwa kuwa na umakini anawamaliza wote, lakini pia tunaacha majonzi makubwa kwenye familia zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la kukinzana kwa sheria mbalimbali; kumekuwepo na kukinzana kwa sheria nyingi sana achana na sheria hizi ndogo, zinakinzana na kukinzana kwa sheria hizi kumeleta changamoto kwenye matumizi, sana. Kwa hiyo pia naomba pamoja na sheria hizi naomba pia ikiwezekana Kamati yako tunaweza kupewa majukumu kuweza kuangalia kukinzana kwa sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kuna sheria kwa mfano, mojawapo ni Sheria ya Madini; Sheria ya Madini inaruhusu madini kuchimbwa popote, Sheria ya Wanyamapori inasema ndani ya hifadhi hakuna kuchimba madini. Sheria ya Ardhi na yenyewe inasema popote panapopatikana madini panaweza kuchimbwa.

Sasa unakuta kuna *confusion*; ndani ya hifadhi haturuhusiwi kuchimba madini, lakini mtu wa madini anaruhusu madini kuchimbwa ndani ya hifadhi, kwa sababu tu ni ardhi. Kwa hiyo sheria kama hizi sasa zinaleta *confusion* na kukinzana, matokeo yake sasa unakuta kwamba ndani ya maeneo ambayo tumeamua kuyalinda tuyatunze tutunze kilichop mule ndani, sheria nyingine imeruhusu anayechimba hatakiwi leo ni mgogoro.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo pamoja na sheria ndogo hizi ambazo zinahitaji marekebisho makubwa na zinaendelea kuangaliwa, pia naomba Serikali iangalie kukinzana kwa sheria mbalimbali, kuhakikisha kwamba kuna *harmonization* ya sheria zote. Kama Sheria ya Wanyamapori inasema kwamba ardhi ya wanyamapori au hifadhi isichimbwe madini, basi iende hivyo hivyo na katika Sheria ya Madini kwamba maeneo ya hifadhi yalindwe yasichimbwe madini. Naomba sana, zipo nyingi sana ambazo kiukweli zikiangaliwa tutaona ni jinsi gani ambavyo zinaweza kukinzana na matokeo yake zinaleta sintofahamu na matokeo yake ni kwamba hazileti *figure* kwa jinsi ambavyo inatakiwa iwe.

Mheshimiwa Spika, yangu ni hayo machache niliyotaka kuchangia kwa leo. Nakushukuru kwa nafasi. (*Makofi*)

SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Magdalena Sakaya. Tutakapokuwa mwishoni mwishoni hapa ambapo tunakaribia kufika, sijui kama Mwanasheria Mkuu utapenda kusema kidogo hapo baadaye, lakini kuhusu hili pendekezo la kwamba kabla sheria ndogo hazijatumika kwamba zipite hapa kwanza, sijui utatushaurije kuhusu hilo. Aahsante sana.

Nilishakutaja Mheshimiwa Lema na Mheshimiwa Taska Mbogo ajiandae.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Tuko ukingoni wa kumalizia Bunge letu kabisa, nafikiri tarehe 19 Mheshimiwa Rais atakuja kulivunja, nami nishukuru kwamba nimepata fursa leo ya kuchangia huu mjadala kuhusu hizi sheria ndogo.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi sipingi kwamba umri una maana kubwa katika maisha, lakini ningeshauri kwa mfano katika hii *Transport License and Public Service Vehicle Regulation* ya 2020 badala ya kuileta kama sheria nafikiri kulikuwa kuna haja ya kupeleka hii sheria kwa wamiliki wa shule maana yake katika hizi *regulations* zingeenda kwenye

Wizara ya Elimu kwa wale wamiliki wa shule wakawa wana-*regulate* wao, ama ikawa ni *some kind of* haraka.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tunaongelea hapa *public schools transport* lakini siku hizi kuna *neighbours* wanaji-*organise* watoto wao au marafiki zao labda wanasoma shule moja wameamua kununua labda *Hiace* halafu wanakubaliana kwamba angalau katika kila wiki hii mke wa Mheshimiwa Ndugai atapeleka watoto shule wiki ijayo mke wa Mheshimiwa Lema atapeleka watoto shule.

Mheshimiwa Spika, sasa wewe mke wako ana zaidi ya 35, mimi mke wangu labda yuko *below* 35, sasa anakamatwa na watoto kwenye gari anawapeleka shule, lakini *families* zimeji-*organise* tu, ni *families* zimekubaliana kwamba watoto wetu wanasoma shule moja, kwa hiyo Mheshimiwa Lema wewe utapeleka watoto wiki hii *next week* atapeleka mke labda wa familia ya Mheshimiwa Ndugai. Sasa anakamatwa kwenye *Noah* mke wangu na ana 27, *traffic* anamsimamisha anamwambia leta leseni yako anamwonesha leseni pale...

SPIKA: Japo sijaiona, lakini nadhani sheria hii inahusu basi la shule, sijui kama inahusu hata kama ukimpeleka kwa bodaboda...

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Spika, nitakueleza madhara yake mbele, kwamba ukishasema basi la shule barabarani watakaoanza sasa kwenda kuitekeleza hii sheria akikukuta na watoto zaidi ya watano ama kumi maana yake yeye atasema hii tayari ni basi la shule kwa sababu limepakia watoto wa shule. Sasa ndiyo nasema italeti shida sana kwenye utekelezaji wake kwa sababu sasa hivi kuna familia nyingi binafsi zinafanya *private organization* ya kupeleka watoto shule, nikiwemo mimi kwa mfano, familia yangu inayo *private organization* na familia nyingine.

Mheshimiwa Spika, sasa nikasema siyo mbaya *issue* ya *age* kwa kweli hata nikiona mtu wa miaka 18 anapela watoto shule kwenye *highway* ninapata wasiwasi lakini

pengine sasa hii Kamati ya Sheria Ndogo ikaangalie namna ya kulileta vizuri zaidi ili isije ikaleta madhara na usumbufu mkubwa huko barabarani, hiyo ndiyo *concern* yangu kubwa kwenye hili jambo.

Mheshimiwa Spika, kuna ishuru ya *line* za simu; simu ni biashara na nitakupa mfano mmoja na naomba sana AG usikilize. Kuna vijana wengi sana wamemaliza chuo wapo mitaani huku wameingia kwenye hizi *crypto currency business* na *forex business*. Kijana mdogo sana ambaye mimi ninaweza nikawa na mfano wa kijana mmoja mdogo sana anaanza na mtaji wa dola 100 kufanya biashara ya kubadilisha fedha za kigeni kwenye mitandao ya kimataifa duniani. Baada ya miezi sita huyu mtu anakwenda mpaka kuwa na mtaji wa 50,000.

Mheshimiwa Spika, *BOT* wakaandika waraka na waliu-*supply* kuhusu *crypto currency* na *forex business* wakakataza M-Pesa, wakaizuia hizi *mobile fund transaction* za Tanzania zisiwe zinapokea miamala ya pesa kutoka kwenye kampuni za *forex* ama *crypto currency*, nini kimefanyika? Hawa vijana kwasababu wameshajua hizi biashara zinalipa, unaanza na mtaji wa dola 100 baada ya miezi sita una dola 60,000 siyo hela ambayo ameiba, ni hela zinazunguka huko duniani kwasababu kwenye soko la *forex* peke yake kuna dola 5.5 trilioni inazunguka kila siku, siyo hela za Tanzania wala siyo za Serikali.

Mheshimiwa Spika, walichokifanya hawakuacha ku-*trade*, wamevuka mipaka wameenda Zambia, wengine *South Africa*, wamechukua line za *South Africa* aidha ni *MTN* ama wameenda Kenya wamechukua *Safaricom* sasa wana-*trade* kwa *line* za Kenya wanarudishiwa *remittance* zao za kigeni kwa hela za Kenya wanatoa pesa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, maana yake ile *remittance* ama faida ambayo walikuwa wanapata *subscribers* wa Tanzania kama *Vodacom is no longer working with our company* na tunapoteza pesa na unajuliza huu uwoga ni wa nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwamba unazuiaje watu wanatoka shuleni kuanza kujua tena dunia ime-*shift*, dunia imetoka kwenye age ya viwanda inakwenda kwenye age ya *information technology*. Huku kwenye hizi *information technology* kuna biashara za mabillioni ya dola zinaendelea kila siku. Kuna mtu na simu yake ya mkononi kila baada ya dakika 10, 15 anatengeneza mpaka dola 1,000 na hawa ni vijana ambao hutowaona mitaani, watakaa ndani na *computer*.

Mheshimiwa Spika, sasa mnavyozidi kuweka vikwazo leo kwamba mtu anahitaji kuwa na *line* moja, watatafuta *option* na *option* nyingine hawa watu watakwenda kwenye nchi ambazo wana uhuru mkubwa wa biashara na mawasiliano. Sasa hoja hapa ni uhalifu, hivi leo fumanizi zikitokea kwenye *guest* kila siku fumanizi 10 utatunga sheria kwamba anayetakiwa kwenda *guest* akionekana na msichana lazima akamatwe?

Mheshimiwa Spika, ninachosema ni kwamba hii sheria ya kusema mtu mmoja line moja, polisi wapo, Usalama wa Taifa wapo na vyombo vya ulinzi vipo; kazi ya Polisi na Usalama wa Taifa ndiyo kuzuia uhalifu kama huu. Sasa kwa nini mnazuia watu kufanya *transaction*/maongezi, amesema Mheshimiwa Salome hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa *minimum* sana Mbunge mmoja anaweza akatumia shilingi elfu 50 kwenye *internet* ama kupiga kwa wiki, kwa mwezi pengine shilingi laki 2. Sasa shilingi laki 1 kwenye simu Serikali tayari ina VAT ya shilingi 18,000 sasa mkiacha watu wakawa na matumizi *regularly* ya simu za mkononi maana yake ni kwamba haya makampuni na Serikali wanapata faida.

Mheshimiwa Spika, sasa wasiwasi wangu ni nini? mnafanya haya makampuni yaone hapa kuna vikwazo vingi vya kibiashara na haya yapo *listed* kwenye *International Stock Market* huko Ulaya. Watakachokifanya tunaendelea kuingia kwenye *chat* ya kuwa Tanzania ni sehemu ngumu na mbaya kabisa ya uwekezaji. Na siyo siri kwamba

telecommunication company sasa hivi zinalipa kodi kubwa katika Serikali hii kuliko kampuni yoyote zile.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nashauri watu waachiwe wamiliki *line*, sheria pengine ingesema hivi na ipo kwamba na nimeona juzi ameshitakiwa mtu kwa kutumia line yake. Ingekuwa ukiruhusu mtu kutumia kitambulisho chako kusajili line na akatumia kwa matumizi, ambazo hizo sheria zipo kwenye *Cybercrime Act*. Lakini kuzuia watu kuwa na *line*, mtu mwingine anaweza akaamua kuwa na line moja akasema hii *line* mimi ni kwa ajili ya *family communication*. Sasa mnasema kampuni moja, hizi kampuni ukienda kuangalia kwa mfano zina *tariff* za *price* zao katika kupiga ama miamala, kuna mtu anaweza akaamua kuwa na *line* tano kwasababu kampuni hii ipo *cheap*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa kinachoenda kutokea mnaua *competition* ya makampuni ya simu na mkia *competition* ya makampuni ya simu, hiki siyo kisiwa watu wataondoka wataenda kufanya *investment* sehemu nyingine ama kama ule mpango wenu wa kama Ethiopia ku-*control* kabisa kila kitu *communication* ndiyo mnataka kufanya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, siku hizi hiki mnachokifanya kwamba tuna-*control* uhalifu; mtu anaweza akashika simu hii aka-*post* kitu sasa hivi hapa halafu akaandika nipo Abidjan na yupo *Dodoma Hotel* hapo, hizi kwenye *computer* huku kuna mambo ya ajabu mno. Kwa hiyo, namna pekee ya kuweza kuzuia uhalifu wa *cyber* siyo kuzuia watu kuwa na *line* nyingi. Mtu anaweza akaingia sasa hivi kwenye *computer*; sasa hivi ninaweza nikaamua nikakupigia simu na *line* ya Marekani na nipo hapa Dodoma hapo *canteen* na ukapokea nikakwambia nipo Marekani, labda walinzi wakwambie waliniona hapa, huo uwezo kwenye hizi *system* zipo.

Mheshimiwa Spika, sasa ukiona sheria kama hizi zinaletwa maana yake watu wetu wa *intelligence* katika mambo ya *cyber* hawapo *smart*. Wakijua jinsi ulimwengu wa

hii *information technology* inavyo-move hamuwezi kufanya hivi ndiyo maana Kigogo mna mwaka wa tano mnamtafuta hamumpati; unaweza ukakuta Kigogo hapa ni Mheshimiwa Zungu au Mheshimiwa Jenister nasema tu mfano labda Mheshimiwa Jenister ndiyo Kigogo... (*Makofi*)

SPIKA: Huo mfano hebu futa bwana

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Spika, nimeufuta... (*Kicheko*)

SPIKA: Afadhali

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Spika, ninachosema ni kwamba tunavyotunga hizi sheria tuangalie madhara yake na nasisitiza sana na Kamati imesisitiza wakati Mheshimiwa Ngeleja anasoma hapa kwamba waacheni watu wawe na uhuru wa kuwa na *line* wanavyotaka ili mradi tu usajili ufanyike na *proper identification* kwamba Lema ana kadi kumi za Vodacom zinasema Lema.

Mheshimiwa Spika, sasa najjuliza polisi wanapenda sana simu zangu; toka nimechaguliwa Bunge hili polisi labda wana simu zangu 10 na line 10. Mnaniambia nikinyang'anywa line na simu, sasa simu yangu ipo Polisi Singida kwa mfano, sasa mnaniambia ikiwa kule Singida nije *TCRA* niandike jamani maombi ya nini na niseme sababu kwa nini nataka *line*, sasa sababu pale naandika simu yangu imechukuliwa na *IGP* Sirro inafanyiwa uchunguzi nili-*tweet* kuhusu mauaji ya Manyoni. *TCRA* sasa sababu ya uoga wanasema ngoja tu-*consult* na *DCI*, *DCI* anasema tukupe muda, nakuwa sina simu? Sasa hiyo mnaweza mkaona ni ya upande wetu, keshokutwa hili Bunge linavunjwa, haya mambo ya kutunga sheria muangalie mbele sana kwasababu yanaweza yasiwaguse nyie yakawagusa ndugu zenu kwa namna moja ama nyingine.

Mheshimiwa Spika, nina simu mpya ipo Polisi Arusha mwaka wa 4, kesi haiishi. Sasa maana yake ingekuwa kwa masharti haya maana yake sitaacha kuwasiliana, nitatafuta

alternative na hiyo *alternative* nitakayoita futa nina uwezo wa kuwasiliana na mke wangu na wewe bila line ya Tanzania. Sasa hii *technology* msiikimbie, msiseme kwamba hii inaleta shida yaani msilogope matusi ya mitandaoni na kukosolewa mitandaoni, tafuteni hoja za kujibu mambo ya mitandaoni mkiona mmepigwa mitandaoni leteni majibu. Sasa mkiwazuia kabisa wataacha kukosoa mitandaoni, wakiacha kukosoa mitandaoni wataanza kukosoa kwa risasi; waacheni watu wapumue wanachosema kama sio ukweli Waziri atoke ajibu. Sasa bahati mbaya...

SPIKA: Tatizo mitandaoni siyo hoja, tatizo ni matusi, uwongo, kashfa ambazo hazipo, hilo ndiyo tatizo halafu tatizo lingine katika mitandao hiyo anasemwa Ndugai nani, Lema hasemwi hata siku moja. (*Makofi*)

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Spika, unamsemaje mtumishi wa Mungu kama Lema?

SPIKA: Halima Mdee hata siku moja hawamsemi wanasemwa wengine tu; ukitazama hilo ukilifuatilia kuna watu yaani hawaguwagi kabisa.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Spika, labda niseme hivi, nyie ni Serikali, sisi tukiwa Serikali tutasemwa kwa kiwango chenu. Nyie ndiyo mnamiliki bajeti, mnapanga matumizi, mna bunduki zote, mna Usalama wa Taifa; sasa siyo Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa, Spika wa Bunge, Waziri Mkuu na wala siyo Mheshimiwa Jenister Mhagama, sasa waliseme kwa lipi? Hata sisi hapa tunapowasema tukigeuka tu tukaja huko tuaanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikisema Bunge linaendeshwa hovy hawawezi kusema Mheshimiwa Lema Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anaendesha hovy, tutakusema wewe. Nikikusema wewe, wewe utakuja kwenye Kamati utanipiga kamati sasa kuna Kigogo humuoni humu, huyo anaweza akapelekewa kwa DM ebwana Kigogo eeh piga hii. Sasa haya mambo wanafanya mpaka wenzako...

SPIKA: Kwanza Mheshimiwa Lema huyu mtu anaitwa Kigogo nimepiga marufuku humu Bungeni asitwaje, marufuku kabisa. (*Kicheko*)

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Spika, sasa nini kinatokea? Sasa watu wengi siku hizi wanakamatwa Kigogo ni nani?

SPIKA: Aah nimepiga marufuku huyo achana naye.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Spika, haya ahsante.

Mheshimiwa Spika, niombe sana hii sheria iangaliwe sana kwasababu italeti shida kubwa siyo tu kwenye *barrier of communication* lakini vilevile kwenye biashara na hata makampuni ambayo yana *advertise*, mmesema kwa mfano kampuni moja iwe na line 30. Sasa hebu *assume* tu wewe una kampuni kubwa inamiliki mtaji wa *over 10 million USD* una watu wa *marketing* zaidi ya 100 na siku hizi unafahamu kwamba mambo mengi yanakwenda *electronics*. Kuna *call business* kwamba kupiga simu kufanya nini unaambiwa kampuni lazima iwe na *line 30*, kampuni yenye mtaji wa zaidi ya dola milioni 100. Hao watasema Tanzania wana *restriction* hata ya kufanya *calls* na *clients*, twendeni nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, sasa wasiwasi wangu ni nini? Hizi sheria tunazozitunga majirani wanaona, wao wata-*easy* masharti kwenye kila namna na ndiyo wataanza kuiba sasa *parts* ya uchumi wetu kwa namna mbalimbali kwenda katika mataifa yao...

SPIKA: Ya pili hiyo...

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe sana kwamba hii sheria ikaangaliwe katika *perspective* ya kibiashara lakini kwamba kuna polisi, Usalama wa Taifa; kama ishuhari imekuwa ni kukamata watu, imarisheni Kitengo cha Polisi cha *Cyber* wapelekeni watu wakasome wawe na uelewa wa kutosha. Ukweli kabisa hata ukiangalia

mambo ambayo polisi wanakimbizana nayo mtandaoni siyo mambo *serious*, ni mambo ya kawaida sana ambayo yangetosha kuwa *ignored*. Yaani kwa mfano kuna mtu ana *tweet* anasema uwogo kabisa anasema Mheshimiwa Msigwa afumaniwa *VETA Hotel*, huyu mtu unakimbizana naye wa nini *if it is not true*. Sasa mnakimbizana katika vitu ambavyo yaani hata ukiangalia vitu wanavyokimbizana navyo polisi ni vidogo. Polisi anatoka hapa...

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Lema, muda haupo upande wako. (*Kicheko*)

MHE. GODBLESS J. LEMA: Eti umeisha Katibu? Ooh!

(*Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

SPIKA: Muda umeisha kabisa, ahsante sana. Kupakazia mtu kafumaniwa wakati hajafumaniwa mbaya sana kwasababu jamii itamuelewa hivyo kwa hiyo anayefanya hivyo lazima afuatwe tu.

Mheshimiwa Taska Mbogo atafuatiwa Mheshimiwa William Ngeleja na baadaye Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Chengo kwa dakika chache halafu tunaanza na upande wa Mawaziri ataanza Mheshimiwa Kwandikwa. Mheshimiwa Taska, Taska hayupo, Mheshimiwa Ngeleja.

MHE. WILLIAM M. NGELEJA: Mheshimiwa Spika, ahsante, nianze kwa kukupongeza wewe kwa kuruhusu hii taarifa ije Bungeni, tunafahamu kwa utamaduni wa kawaida na mazoea tuliyonayo ya uendeshaji wa shughuli za Bunge, wakati huu wa Bunge la Bajeti huwa ni Bunge maalum kwa bajeti sasa tunakushukuru kwa kutupatia fursa kuiwasilisha hii taarifa na manufaa yake kama inavyoonekana. Yapo mambo ambayo...

SPIKA: *Actually* Mwenyekiti nikukumbushe hii ndiyo Kamati peke yake katika Bunge ambayo huwasilisha taarifa zake mara mbili kwa mwaka, hakuna Kamati nyingine yeyote,

ni Kamati ya Sheria Ndogo peke yake. Endelea tu na mchango wako. *(Makofi)*

MHE. WILLIAM M. NGELEJA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana na sisi kwa kweli hilo limetutia moyo lakini limetufurahisha sana na ndiyo maana tumefanikiwa kupitia hizi sheria 2601 ambazo miongoni mwake zenye kasoro zilikuwa hizo 547 kwa hiyo, la kwanza lilikuwa ni la kukushukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, kuwezesha huu mfumo wa uendeshaji wa Bunge kwa Bunge Mtandano umetusaidia sana, tunajua umesaidia Bunge zima lakini sisi kwa Kamati yetu ya Sheria Ndogo kwasababu kwa asili ya kazi yake ni uchambuzi wa makaratasi kabla ya huu mfumo wa ki-*digital* ilikuwa kazi kubwa sana. Tunakupongeza sana wewe na pia tunampongeza Mtendaji Mkuu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa kazi kubwa mliyoifanya, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa ujumla kwa hiyo hekima na busara mkafanya maamuzi tuingie kwenye Bunge Mtandao mapema kadiri ilivyowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mengi yamesemwa na nisingependa kuyarudia kwa ababu taarifa inajieleza lakini nilitaka kuzungumzia machache ya msisitizo na kukumbusha tu. Moja, nilitaka ku-*share* na Waheshimiwa Wabunge hapa kwamba haya mapendekezo yanayoonekana kwenye taarifa yetu kimsingi tumeshayashauriana na Serikali na ninaweza kusema kwa kiasi kikubwa kama siyo yote kabisa tumekubaliana na Serikali kwamba yakafanyiwe marekebisho kama ambavyo tumependekeza na kushauri kwenye taarifa yetu. Kwa hiyo, maeneo mengi hapa hayabishaniwi sisi na Serikali.

Mheshimiwa Spika, na kwa nafasi hii nilikuwa napenda kwa niaba ya Kamati tuishukuru sana Serikali kwa ujumla wake; Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri pamoja na watendaji ambao wamekuwa wakipata nafasi ya kuja kujadiliana kwenye Kamati yetu. Mara nyingi tumekuwa na mijadala ya kina lakini kikubwa tumekuwa na maridhiano ya

hali ya juu sana na unafahamu kwa sababu mara kadhaa huwa tunakushirikisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi tunaishukuru sana Serikali kwa kuelewa Kamati yako na hata kwenye mambo ambayo yamekuwa ni magumu na wakati mwingine imekuwa ni changamoto kweli lakini wanasema penye wengi huwa haliharibiki neno na ndicho ambacho kimekuwa kikitokea kwenye Kamati yetu. Kwa hiyo, mambo mengi haya yaliyopo kwenye taarifa yetu tumeshaelewana na Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jingine ambalo nataka nisisitize hili tulilolizungumza kwamba haya marekebisho yatakayofanywa kwanza tumependekeza na kushauri kwa Serikali kwamba Serikali ikafanye haraka sana marekebisho haya ya dosari tulioziona halafu ikishakamalisha utaratibu wa kawaida haya marekebisho yapitie kwenye mfumo wa kawaida wa Kiserikali yakachapwe kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali halafu baadaye tumeshauri kwamba hiyo taarifa ije Bungeni.

Mheshimiwa Spika, nataka niliweke wazi jambo hili kwa namna ambavyo mfumo wetu ulivyo na usisumbue Waheshimiwa Wabunge wenzangu wanaoendelea kuchangia. Jambo hili kwa mfumo tulionao hizi Sheria Ndogo zinapotungwa kwa mfumo tulionao, zikishatungwa hata kabla hazijajadiliwa na Kamati zinaanza kutumika, ni mfumo tulionao na haiwezekani ikawa mjadala leo tufungue kwamba zisitumike.

Mheshimiwa Spika, tulichokishauri na tulichoelewana na Serikali kwamba wakishakamilisha huo mchakato wa marekebisho yote baadaye wataleta hapa Bungeni kwa taarifa na Kamati hii si lazima iwe na *composition* hii lakini kwa Bunge lijalo litajiridhisha kwamba katika hali yake ya kawaida tu kwamba haya yalitokea mwaka fulani na baadaye yakafanyiwa marekebisho na sasa yamenyooka kwa kadiri ambavyo Serikali na Bunge lako walishauriana. Hatukukusudia kusema zisitumike kwanza kwa sababu huo

sio mfumo wetu, mfumo wetu ni kwamba zikishafanyiwa marekebisho ziendeleo kwasababu ndiyo utaratibu wa kawaida wa mfumo tulionao. Niliona kwamba ni jambo la msingi kusisitiza hili jambo lieleweke vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maelezo mengine ambayo tulitaka kusisitiza, moja ni la uzingatiaji wa masharti ya msingi. Masharti ya msingi moja ninayozungumzia moja ni kuhusu Sheria Ndogo ama Kanuni zinazovunja haki za binadamu. Sasa wenzangu wameshazungumza lakini huko kwenye mijadala kumekuwa na mambo ambayo nyakati zingine yanashtua kidogo kwasababu yamekuwa yakija mambo mengine mazito sana, unajiuliza hili lilipitaje katika mfumo wa kawaida ndiyo maana tunalisisitiza hapa kuliweka kwenye taarifa zetu rasmi kwamba Serikali iendeleo kuwa makini sana katika maeneo haya ambayo baadhi ya vifungu katika hizi kanuni zinazotungwa zinakuwa zinakiuka misingi ya haki za binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo, nilikuwa napenda kusisitiza hili la elimu kwa Umma kama walivyozungumza; Mheshimiwa Dau, ahsante sana na wengine waliozungumza. Mahususi kwa taarifa hii. Yale masuala yanayohusu leseni za watoa huduma ya magari pamoja na sheria zake na kanuni zake za uendeshaji, hayo ni maeneo ambayo yaliibua mijadala mzito sana. Hili ni eneo ambalo tunalisisitiza kwa msisitizo wa pekee.

Mheshimiwa Spika, Serikali kimsingi tulishakubaliana kama nilivyosema, waende kutoa elimu kwa Umma. Kwa sababu lilikuwa na mambo mazito sana ndani yake. Haya ni machache kwa sababu tusingeweza kuyaleta yote hapa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ndiyo maana tunasema elimu kwa wadau ni muhimu sana kwa walengwa, waathirika, Umma kwa ujumla ufahamu kwa sababu kuna wajibu na haki za watumiaji tukadhani kwamba hili ni eneo ambalo linahitaji kupewa jicho la kipekee na katika kipindi hiki ambacho kanuni zinakwenda kurekebisha basi jambo la kutoa elimu kwa Umma na lenyewe lipewe umuhimu wake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, nirudie tena kusema wewe na Serikali mlishauriana vizuri sana kuirudisha hii Kamati ya Sheria Ndogo kwa sababu kama unavyoona, ingekuwa inaning'inia kwenye mojawapo ya Kamati nyingine, inawezekana kabisa tusingeweza kuwa tunafanya uchambuzi wa kina. Kwa hiyo, tunakushuru sana wewe na wasaidizi wako wote; Naibu Spika, Wenyeviti na Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kiutaratibu, kuna wakati hizi Kamati mnashauriana ziundwe, lazima kuna hizo *consultation*. Huu ulikuwa ni uamuzi mmojawapo wa msingi na wa heshima na faida kubwa sana kwa Taifa letu. Tunaamini kwamba Bunge lijalo pia hii Kamati itaendelea kusimama kama ilivyo kwa ajili ya kusaidiana na Kamati nyingine kufanya yaliyo mema kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu ni shukrani kwa Mheshimiwa Mtemi Andrew Chenge, Mwenyekiti wetu. Huwa tunasema tunaendelea kufaidi sana kama Bunge la Jamhuri, kama Watanzania nasi ambao tuko kwenye Kamati hiyo tunaendelea kufaidika zaidi. Alivyosema Mheshimiwa Mlinga na wengine, hiki kimekuwa ni kisima; tunashukuru kwamba Serikali tunapokuwa tunakutana tumekuwa tukirahisisha na mambo magumu yanakuwa rahisi sana kwa sababu, pamoja na mengine, weledi wa Mwenyekiti wetu, Mheshimiwa Mtemi Chenge na Kamati kwa ujumla, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti imefanya kazi kubwa mno. Sisi kwenye Kamati yetu pale, kama unafahamu mfumo wa utendaji kazi wa Kamati hizi, mambo yanaanzia kwenye Sekretarieti. Sekretarieti yetu, sitaki kurudia kuwataja majina lakini wanafanya kazi kubwa. Naamini hii inatokana na msimamo pia wa Mtendaji Mkuu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai kwa namna ambavyo anasimamia hizi Kamati. Hongereni sana na tunaamini kwa pamoja tutaendelea kulijenga Taifa letu kupitia hizi kanuni ambazo zinawagusa wananchi moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati nahitimisha niseme tu kwamba sisi Kamati yako tuko tayari kwa mara nyingine, kadri Mwenyezi Mungu atakavyojaalia tukutane hapa mwezi wa 11, tupo tayari kuendelea kuhudumu kwenye Kamati hiyo bila hofu yoyote kwa sababu kama uzoefu ni Walimu bora, basi sisi tumeshakuwa Walimu katika hili eneo kwa sababu niyaraka sasa hazitusumbui kuzipitia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ngeleja. Nimepata mawasiliano hapa kwamba Mheshimiwa Chenge atahitimisha, kwa hiyo, nitamwita mwishoni kabisa Mheshimiwa Naibu Waziri Kwandikwa, karibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi, nami niweze kuchangia kwenye hoja ya Kamati ya Sheria Ndogo. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mungu ambaye ameniwezesha kusimama mbele yako niweze kusema kidogo.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru wewe kwa umahiri wako, naona Kamati imefanya kazi nzuri, lakini kwa utashi wako wa kuwa na Kamati hii ya Sheria Ndogo, nina uhakika kwamba inatengeneza ile *mechanism* ya *check and balance*. Kwa sababu tutakapokuwa na kanuni au sheria halafu Kamati hii inapitia, kuna maboresho makubwa ambayo upande wa Serikali tunayafanya. Kwa hiyo, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Kamati kwa sababu wakati tulipokwenda kwenye Kamati, mijadala ilikuwa na afya kweli. Yako mambo ambayo tuliyatolea ufafanuzi, kimsingi Kamati iliyakubali, lakini yako mambo ambayo Kamati ilikuja na maelekezo na ushauri, nasi kama Serikali tuliyakubali, matokeo yake tumepata taarifa hii nzuri kabisa.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba baadhi ya wachangiaji ambao wengi ni Wajumbe wa Kamati hii wamezungumza mambo ambayo wakati mwingine pia tulikuwa tumeshaya-*exhaust* kwenye Kamati. Kwa hiyo, nitazungumza kwa uchache tu, lakini kimsingi yale ambayo tulikuwa tumekubaliana kwenye Kamati kwa nia thabiti ya kuboresha kanuni zetu kwamba tulikubaliana, nasi kama Serikali tunaenda kuyafanyia kazi kwa haraka ili tuweze kuyaboresha ili yaweze kuleta manufaa makubwa katika matumizi ya kanuni hizo.

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa suala la usafiri hususani madereva wa magari ya wanafunzi. Nakushukuru binafsi kwa sababu hata wakati uki-*chip in* ulizungumza na kuona kwa yale ambayo pia yametokea. Niseme tu kwamba katika kuiangalia kanuni hii, tumezingatia pia sheria nyingine, lakini mwisho wa safari kuna maboresho ambayo tutayafanya kwa lengo hilo hilo kwamba yanatupeleka kwenye umri ule ambao tulikuwa tumekubaliana.

Mheshimiwa Spika, tumeona kwamba *studies* mbalimbali zilizofanyika kutokana na ajali zinaonyesha kwamba asilimia karibu 80 ya ajali zilitokana na tabia za kiutu na hasa tumeona ajali nyingi zilitokana na umri. Sasa nasi kama Serikali tulikuwa tunalionga hilo kwamba ni vizuri tuliwekee utaratibu mzuri ili kuweza kuwalinda watoto wetu wakiwa kwenye usafiri wa wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, mfano ile ajali iliyotokea kule Arusha, yule dereva kama sikosei alikuwa ana miaka 22. Pia ziko ajali nyingi tu kwenye utafiti uliofanyika, inaonyesha kwamba umri pia ni suala la kuzingatia tunavyokuwa tunawapa leseni hawa madereva. Kwa sababu ukiangalia sheria yenyewe ya leseni ya udereva, kwamba mtu anapewa leseni akiwa na miaka 18; anatakiwa kupewa leseni ya kuendesha gari ya abiria akiwa ametumika kama miaka saba akiwa na miaka 25.

Mheshimiwa Spika, tulikubaliana tufanye marekebisho kwamba mtu aliyeendesha gari ya abiria kwa miaka 10

inampeleka kwenye miaka 35 ili aweze kuendesha gari ya watoto wadogo. Kimsingi tulikubaliana na Kamati lakini msingi wake ni huo kwamba tunapenda tuone watoto wetu wakisafirishwa wakiwa salama kwa sababu ziko tabia nyingine kutokana na umri watu wanaweza kupata jazba wakiwa wanahudumia hawa watoto. Kwa hiyo, tunakwenda hivyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, yale mengine ya kuongeza kama vigezo kama nilivyozungumza kwamba uzoefu tuweze kuuongeza kule kwenye kanuni yetu tuweze kuboresha zaidi ili watu waingie kwenye utaratibu kwa kufuata kanuni; lakini tulikuwa tunaona kwa kweli kwa miaka 18 mtu kuanza kuendesha gari ya watoto, wakati mwingine haikuwa sahihi sana kwamba tujipe muda kidogo mtu kupata uzoefu na hiki ndiyo kigezo ambacho pia tunakiona katika kuweka watoto wawe katika hali ya usalama.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hii tutaiweka tu vizuri na kwa haraka ili iweze ku-*accommodate* tuone watoto wetu wanaweza kupata huduma vizuri wawe salama zaidi wakiwa wanaenda kwenye masomo yao. Kwa hiyo, hii tunakwenda nayo hivyo vizuri.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine limezungumzwa hapa la usajili wa laini. Tumeanza zoezi la usajili kama unavyokumbuka, lakini tunajaribu kuangalia kwa takwimu, labda niweke takwimu kidogo kwamba tangu tulivyokuwa tumeanza kusajili laini tulikuwa tunategemea kusajili laini milioni 48, lakini mpaka ninapozungumza, laini milioni 43 zishasajiliwa kuonyesha laini kidogo milioni tano zilizobaki inawezekana kuwa ni zile ambazo watu walikuwa wameweza kumiliki laini nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, ni kweli kwamba tunahitaji kuwa na uhuru wa kuwa na laini hizi, lakini ni vizuri pia uhuru ukawa na ukomo. Wako watu walikamatwa; mtu ana laini 600. Sasa fikiria kwa laini ya mtandao mmoja mtu awe na laini 600, kweli atakuwa na nia njema na sisi! Kwa hiyo, nilikuwa nasema, hata Waheshimiwa Wabunge

watakubaliana name kwamba wapo watu ambao wana laini kawaida lakini alienda akasajili laini kwa ajili ya *tab*, ana laini labda ya *iPod* alikuwa nayo. Akitoa maelezo kwa muda wa dakika tatu, Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, wamesajili laini zaidi ya moja kwenye mtandao mmoja, lakini lazima zile sababu ziweze kujulikana.

Mheshimiwa Spika, tunachokisema ni kwamba lazima kuwepo na udhibiti ili pia tuweze kuweka *data* vizuri kuona matumizi mazuri ya laini hizi. Kwa hiyo, suala la kusajili kwa haraka tumelizingatia kwenye kanuni na suala la kuona kwamba tunakuwa na udhibiti ili sasa matumizi ya laini yaweze kutusaidia kuwa salama zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaona kabisa lengo ni zuri na lengo letu ni kuhakikisha kwamba tunadhibiti uhalifu wa kimtandao na hii inaonyesha, kwa sababu hata sasa rekodi hizi zinaonyesha uhalifu wa kimtandao umepungua.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo bado ziko changamoto nyingine. Ukiangalia kwa mfano kama tutaruhusu kila mtu asajili laini, wapo watu wengine wanaweza wakatumia hata vitambulisho vya watu walioko kule vijijini kutokana na elimu yetu ambayo tunaendelea kuipeleka kidogo kidogo kufundisha watu waone umuhimu wa kuwa na hizi laini, mtu anaweza akawa na laini amesajili kwa kitambulisho, lakini bado ametumia watu wengine ambao hawana uelewa akawaingiza watu wengine kwenye matatizo ya uhalifu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naamini mlango upo kwamba kadri tunavyokwenda kufanya maboresho, tunaamini kabisa yako mambo mengine tutaendelea kuyaboresha kadri tunavyokwenda. Kwa hali ilivyo sasa, tunaruhusu kama kuna mtu anaweza kwenda mpaka laini 30 kwa kibali maalum, akaomba na sababu ya matumizi, bado mamlaka itamsajili. Kwa hiyo, utaratibu tulionao uko vizuri na haunyimi uhuru wa mtu. Ninaamini kabisa kwamba kama taratibu zitafuatwa, bado wananchi wanaweza kuendelea kupata huduma hii ya kupata hizo laini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme yale ambayo tuliyazungumza kwenye Kamati tumekubaliana tutaenda kufanya marekebisho. Pia suala la kufanya kazi kwa ubora na kwa uharaka kwa maana ya utaratibu wetu wa kusajili laini kwa dakika tatu, tunaweza kwenda kufanya hivyo. Kama kuna mtu atakuwa na sababu maalum aitoe, kama Mheshimiwa Makamba, ametoka hapa, hata nilikuwa najaribu kuangalia pia naye ana laini za kutosha hapa; kwa hiyo, nilikuwa nimejaribu ku-*access* kuona kwamba anazo laini, lakini ile kusema kuwa na laini bila ukomo, wakati huu siyo vizuri. Ni vizuri tufuate taratibu na hakuna kikwazo cha kuwa na laini hizi, lakini cha msingi tuone kwamba tunaenda kutumia laini hizi vizuri bila kuwa na mashaka yoyote.

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge waliochangia. Kama ilivyokuwa kwenye Kamati, Mheshimiwa Mwenyekiti yuko hapa, kuna wakati mwingine tulikuwa na pande zote mbili; kuna wengine ambao wali-*support* upande wa Serikali, wengine walirudi upande mwingine, lakini kwa hili namshukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti kwamba aliongoza mijadala vizuri sana, tumekuja na mapendekezo mazuri sana ambayo tumeyapokea kama Serikali. Makamu wa Mwenyekiti pia kwa umahiri wake na uzoefu wake ninamshukuru sana. Wajumbe wote wa Kamati tulikwenda vizuri kupitia kanuni hizi.

Mheshimiwa Spika, nirudie kukushukuru tena kwa nafasi hii, nami kwa kweli nilipokuwa kwenye Kamati nimeendelea kujifunza, mimi siyo Mwanasheria lakini nimeona namna nzuri uchambuzi ulivyokuwa unafanywa, naomba sana Kamati hii Mungu awabariki waendeleo kutusaidia katika kuboresha shughuli mbalimbali za kanuni zetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii.
(*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kwandikwa, Naibu Waziri nakushukuru sana. Sasa nimkaribishe Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, karibu tafadhali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hoja iliyoko Mezani ambayo ni taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuhusu uchambuzi waliofanya na yale waliyoyaona katika uchambuzi wao.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwapongeza sana Kamati hiyo, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Chenge kwa kazi kubwa ambayo wameifanya ya kuchambua hizo sheria ndogo zote na haya yote ambayo wameyaona na ambayo wametushauri.

Mheshimiwa Spika, nianze kuelezea suala la uwepo udhaifu katika utengenezaji wa sheria ndogo. Jibu letu ni kweli, tunakubali kwamba upo udhaifu mbalimbali katika utengenezaji wa sheria ndogo na ndiyo maana tumekuwa tunachukua hatua mbalimbali ya kuweza ku-*address*udhaifu huo. Mifano imetolewa mingi sihitaji kurudia; makosa ya kiuandishi, masuala ya sheria ndogo kupingana na sheria mama, pamoja na ukiukwaji wa misingi mingine, tumeyaona hayo yakitokea, changamoto hizo zipo.

Mheshimiwa Spika, labda niseme tu kwamba uandishi wa sheria ni kitu *technical*/kidogo, ndiyo maana hata wakati mwingine Bunge hili hili linatunga sheria zake lakini linaenda kupimwa kwenye mizani ya Mahakama, nazo zinasema tena kitu kingine na kadhalika. Kwa hiyo, siyo jambo ambalo linapaswa kutuogopesha sana na kututisha sana, lakini ni jambo ambalo tunapaswa kulifanyia kazi. Maoni yote ya Kamati nafikiri yamechukuliwa na yanafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, nilipenda niongee kidogo, kwa nini changamoto hizi zinajitokeza? Suala la Uandishi wa Sheria, tunaita ni taaluma mahsusi ndani ya taaluma ya sharia. Yaani una taaluma ya sheria lakini ndani ya taaluma hiyo ya sheria tena una taaluma ndogo mahsusi ambayo inahusu Uandishi wa Sheria Ndiyo maana huwa ni lazima pia kutoa mafunzo maalum kwa ajili ya uandishi wa sharia, mafunzo ambayo kwa kawaida huwa hayatolewi katika vyuo vyetu.

Mheshimiwa Spika, uliligusia hilo kidogo, hiyo ni changamoto. Wanafunzi wetu wanapokuwa katika vyuo wanafundishwa *Legal Writing and Drafting* lakini uandishi wa sheria ni *Legislative Drafting*. Tukija kwenye vyuo kwa mfano ambavyo vinafundisha taaluma hii, tunavyo vichache sana. Sisi hapa tuna-*train* watu wetu zaidi Uingereza, ndiko kuna vyuo vya kuaminika na kidogo Zambia. Katika Ukanda wote wa Afrika ni Zambia na nje ya Afrika ni Uingereza. Kwa sababu kuna *technical complications* nyingi sana katika taaluma hiyo. Kwa hiyo, hiyo ni mojawapo ya changamoto na ndiyo maana waandishi mahiri wa sheria tunao wachache kabisa.

Mheshimiwa Spika, sasa tunafanya nini? Nilishazungumza hili katika vikao vilivyopita nikasema tumepanga mpango wa mafunzo walau ile *elementary training* na nilieleza kwenye lile Bunge mwezi wa Pili kwamba tulikuwa tumeshapanga mipango ya kuanza mafunzo haya, kwa kweli isingekuwa shida ya *COVID 19* tungekuwa tumefanya. Tulipata *support* kutoka *African Legal Support Facility* na fedha hizo tuliomba tuelekeze katika ku-*train* wanasheria wetu, siyo tu kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali lakini kutoka kwenye Wizara mbalimbali, taasisi mbalimbali, Halmashauri na kadhalika, hata Wanasheria wa Bunge na hata Wanasheria wanaofanya kazi za kiutawala katika mhimili wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, pia tulipata fedha nyingine kutoka *World Bank* ambazo zilipitia Mahakama na zenyewe zipo kwa ajili ya *training* hiyo. *Training* hizi zote kama nilivyosema zimeshindwa kufanyika kwa sababu ya hii changamoto iliyojitokeza. Pengine sasa baada ya hali hii kuwa inabadilika kidogo, tunaweza tukaanza hizo *training* ambazo zilipaswa kuwa zimefanyika.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine katika eneo hili, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeandaa mwongozo wa mambo ya kuzingatia katika utengenezaji wa sheria ndogo na mwongozo huu tuliushirikisha kwa Wakurugenzi wote wa Idara za Sheria kwa sababu sasa hivi wanasheria wote wa Serikali wanaangaliwa na kusimamiwa na Mwanasheria Mkuu

wa Serikali moja kwa moja. Naomba tu nilitaarifu Bunge lako kwamba kufikia mwisho wa mwezi huu tutakuwa tume-*gazette* huo Mwongozo ambao tunatumaini kwamba utasaidia sana kuwaongoza wale wote wanaofanya hiyo kazi ya kuandaa hizi sheria ndogo ili tuweze kuepukana na hizo changamoto mbalimbali ambazo zimejitokeza.

Mheshimiwa Spika, pia tunaendelea kusesitiza kwamba utengenezwaji wa sheria zote ndogo ni lazima uishirikishe Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kwa hiyo, zinaletwa kwetu baadhi na baadhi tunahitaji bado kuendelea kuwakumbusha kwamba hizo sheria ni vyema zikaletwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuangaliwa na kama kuna changamoto. Kwa wale ambao wameleta, tumeweza kuondoa zile changamoto kabla hata hazijawa *published* hizo sheria na hazijaanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, labda jambo la mwisho niongelee hili pendekezo la Bunge kuziangalia hizi sheria ndogo na kuzipitisha kabla ya kuanza kutumika. Ninaelewa *frustration* iliyopo nyuma ya pendekezo hili kwamba pendekezo hili linatokana na changamoto ambazo zimeonekana. Ila tuisahau kwamba utungaji wa sheria ndogo kwa mamlaka mbalimbali kwa njia ya kukasimiwa mamlaka hayo na Bunge, unatokana na msimamo ulio katika sheria na katika Katiba hasa Ibara ya 97(5). Kwa mujibu wa ibara hiyo, basi Bunge linakasimu madaraka yake hayo ya kutunga sheria.

Mheshimiwa Spika, sasa changamoto iliyopo ni ile *concept* ya *delegated legislation*, yaani ile dhana nzima ya kukasimu mamlaka ya kutunga. Katika sheria ya kiutawala (*Administrative Law*) unapokasimu madaraka unaruhusu yule uliyemkasimisha kuyatekeleza yale mamlaka na umekuwa umekwenda na kinyume na msingi ule na dhana ile halafu baadaye ukaja kuyachukua na kulisimamia jambo lile utakuwa kimsingi umepingana na ile dhana zima ya kukasimu madaraka na kwa hiyo hata kwenye kukasimu madaraka yakutunga sheria ni hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwamba ukiyakasimu yale madaraka unatumaini kwamba huyu mtu ataongozwa na ile misingi katika kuya-*exercise* yale madaraka na kwa hiyo atafanya jambo katika utaratibu ambao unakubalika. Na ndiyo maana, katika misingi ya sheria ya utawala pale ambapo yule aliyekasimiwa madaraka amekwenda kinyume au akufuata misingi ya kufanya jambo lile basi *remedy* yake ni *Judicial Review*. Kwa hiyo ni kwenda mahakamani na kuomba kwamba ifanyike *Judicial Review* na kwa *situation* hii itakuwa ni *Judicial Review of a Delegate Registresion* na misingi yake ipo. Kwamba sheria ipo imekuwa imekizana na Sheria Mama inaitwa *doctrine of ultra-vires*, kwamba sheria iliyotungwa ni *Ultra-vires the Principle Regrestration*

Mheshimiwa Spika, na ndiyo maana hata katika sheria ilivyo sasa hivi hili suala la kukasimu madaraka ya kutunga sheria kwa Bunge limeelezwa vizuri katika Sheria ya Tafsiri ya Sheria (*interpretation Laws Art Chapter One*) Kifungu cha 38 (1), ambacho kinasema sheria zote hizi zitaletwa Bungeni kuangaliwa baada ya kuwa zimekuwa *packed* na kifungu cha 37 kinasema pale unapo-*published* ile Sheria Ndogo ndipo itaanza kutumika. Kwa hiyo kimsingi kifungu cha 38 kinachosema ni kwamba sheria hiyo italewa hapa ikiwa imeshaanza kutumika. Na kama nilivyosema mwanzo hiyo inaendana na *consept ya delegated registration* vingine ukifanya kinyume cha hapa unakuwa umeifunja hiyo *consept* nzima.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nafahamu kama hilo wazi pengine litakuwepo ni lazima kurekebisha kifungu hiki, lakini kama ninavyosema tena kwa mara nyingine kwamba kufanya hivyo tutakuwa tumevunja misingi iliyopo. Nadhani cha muhimu na kwa ushauri wangu tuyafanyie kazi au tusifanyie kazi hizo changamoto ambazo zimeonekana. Na kama nilivyosema tunazikubali tunazipokea na hatua zipo tayari zimeshaanza za kuzifanyia kazi hizo changamoto mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, vinginevyo nimalizie tena kwa kuishukuru na kuipongezaKkamati ya Sheria Ndogo kwa kazi

kubwa ilivyofanya na sisi tutaendelea kushirikiana nao katika kuhakikisha kwamba sheria zetu zinakaa viziuri.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Sasa nikuute Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista Mhagama tafadhali, baada ya hapo mtoa hoja.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, mimi nasimama hapa kwa niaba ya Serikali; kwa kuwa hii ni taarifa ya mwisho ya Kamati ya Sheria Ndogo kuwasilishwa katika Bunge lako la Kumi na Moja; kwa kweli kwa niaba Serikali ninaomba nitoe shukrani za dhati kabisa kwa Kamati hii ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa ambayo wameifanya katika kipindi hiki cha miaka mitano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mujibu wa Kanuni za Bunge imepewa jukumu hilo la kupokea maagizo na majedwali kutoka katika Kamati ya Sheria Ndogo mara baada ya Sheria Ndogo hizo kuwa zimewekwa mbele ya Bunge lako Tukufu. Kwa hiyo kazi hii imefanyika na ofisi yangu na mimi binafsi nimekuwa nikiwawakisha Mawaziri wote ku-*appear* kwenye kamati ya Sheria Ndogo na kuyapokea yale yaliyojili katika Sheria Ndogo ambazo nimekuwa nikiziwasilisha Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naomba niungane mkono na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, lakini vile vile niungane mkono na Mwenyekiti wa Kamati, Makamu Mwenyekiti na wajumbe wa Kamati, kwamba ni kweli kabisa yapo maeneo ambayo yalikuwa ni maeneo tata kweli kweli katika Sheria zile Ndogo ambazo tulikuwa tunaziweka mezani na wakati mwingine zilikuwa zinafanyiwa kazi na Kamati ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Spika, sasa kwanini nasemakwamba tunaishukuru sana Kamati hii; katika kipindi hiki cha miaka mitano Sheria Ndogo takribani 2,601 zimefanyiwa kazi na

Kamati hiyo, na kwa kweli ukikuta Kamati ipo kazini na ulikuwa unaona jinsi Kamati ilivyokuwa *busy* kufanya hii kazi. Mara zote wamezungukwa na karatasi na hizo sheria mama na Sheria Ndogo; kwa kweli walikuwa makini kweli kweli na wamefanya kazi zao kwa umakini wahali ya juu.

Sheria Ndogo hizo ambazo zilikuwa zinapitawa na Kamati hiyo ilikuwa ni pamoja na kanuni za Wizara mbalimbali ambazo ni *regulations* kutokana na sheria ambazo tulikuwa tumezitunga; lakini kulikuwa na amri (*orders*) ambazo zimetengenezwa taasisi mbalimbali za Serikali, kulikuwa na matangazo (*notices*) ambazo zikuwa zimetolewa na Serikali na taasisi mbalimbali. Vilevile kuliwa na kanuni za taasisi (*rules*) ambazo zilikuwa zimetengenezwa kupitia Serikali, kulikuwa na matamko mbalimbali ambayo yalikuwa yanawasilishwa mbele ya kamati hiyo. vitu hivi vyote kwa ujumla wake ndiyo unaona kwamba vinalea taswira ya ukubwa wa kazi ambazo zilikuwa zinafanya na Kamati hii Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Spika, kwahiyo kwa unyenyekevu mkubwa kwa niaba ya Serikali tunaishukuru sana kamati hii, imefanya kazi ya kizalendo ikiongozwa na Mwenyekiti wao, ndugu yangu Mtemi Chenge, lakini vilevile Makamu Mwenyekiti ndugu yangu Mheshimiwa William Ngeleja na Wajumbe wote wa Kamati. Hawa akina Mheshimiwa Mlinga usiwaone hivi, kwenye ile Kamati walikuwa wanatuoja jasho kweli kweli na walikuwa wanatuweka kitimoto kweli kweli ili mambo haya yaweze kwenda vizuri; kwa hiyo kwa kweli tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, sitaki kurejea sana sana katika yale ambayo Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameyatolea ufafanuzi. Hata hivyo niseme, ukiangalia *trend* ya mapokea ya Sheria hizi Ndogo 2,601 kwa kipindi hizi ambacho Bunge lako Tukufu na Serikali tumeyafanyia kazi, na zile zilizokutwa na sodari hizo 547; ukiangalia mwenendo huu na ilivyokuwa mwanzo nadhani Mtemi Chenge anaweza akakungana na mimi. Huko mwanzo hali ilikuwa ni mbaya zaidi, lakini kwa sababu Kamati hii iliendelea kutupa elimu iliendelea kutusaidia kuwa ni jicho letu la pili haya marekebisha na ubora

wa hizi sheria ndogo viliendelea kufanyiwa kazi mara kwa mara na kurekebishwa kasoro nyingi ambazo zilikuwa zinajitokeza katika sheria hizi.

Mheshimiwa Spika, *commitment* yetu nini ndani ya Serikali. Ni kuendelea kwanza kuithamini kamati hii ndogo kama jicho letu la pili la kujipima nakujitathimini. Nina kuhakikishia kabisa Mawaziri wenzangu ambao walikuwa wanapokea yale majedwali niliyokuwa nayawasilisha kwao kwa kweli waliona umuhimu wa uwepo wa Kamati hii katika kuifanya Serikali itekeleze majukumu yake sawa sawa. Na jinsi kamati ilivyokuwa inatushauri kuna maeneo ambayo tulikuwa tuna-*compromise* kwanini Serikali imeamua kuweka vifungu hivyo, na kuna maeneo ambayo kwa kweli tunaona hapa sasa ni *give and take* lakini kuna maeneo ni lazima tuyoandoe. Kwa hiyo tumekwenda hivyo na ninaamini msaada huu una tija kubwa sana kwa wananchi wa Tanzania kwa ujumla wake katika eneo hili la matumizi ya Sheria Ndogo ambazo zinatokana na Sheria Mama zinazotungwa kwa mujibu wa Katiba na Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mambo makubwa mawili ambayo Kamati imeishauri Serikali yetu na tunatakiwa kuondoka nayo hapa; na mimi kama Msaidizi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ndiye Kiongozi wa Shughuli zote za Serikali hapa Bungeni ninaomba kuliahidi Bunge lako Tukufu kwamba tutakwenda kuyafanyia kazi. Mwanasheria Mkuu hapa ameeleza vizuri.

Mheshimiwa Spika, ya kwanza imesisitizwa sana utoaji wa elimu kuhusu masuala haya ya sheria ndogo. Lakini na Sheria Ndogo zenyewe ambazo zimeshatungwa. Eneo hili tutakwenda kulifanyia kazi sana; tutapeana maelekezo ndani ya Serikali, kila idara, Taasisi na Wizara baada ya kuwa imekamilisha utungwaji wa Sheria Mama kupitia Bunge, kanuni na sheria hizo zote nyingine, iwe ni *order, rules* ama ni *regulations* kuna haja ya kutoa elimu ya matumizi ya sheria hizo; katika maeneo ambayo yanatakiwa kutumika

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo jambo hili nadhani ndani ya Serikali tutazungumza na tutalifanyia kazi. Kwa sababu wakati mwingine watu wamekuwa wakizivunja pia hizi Sheria Ndogo bila kujua kama zipo. Kwa hiyo kuna haja ya kufanya kazi ya uelimishaji.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kubwa, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali amelitolea maelezo, na mimi naomba kukuhakikishia tutalifanyia kazi ni hili la kufanya marekebisho katika zile Sheria Ndogo ambazo mimi nilipokea majedwali yake na kuyawasilisha kwa Mawaziri mbalimbali; naomba nikuhakikishie kwamba hatua hiyo imesha anza. Takriban kila taasisi na Wizara wameshapitia yale majedwali na kuanza kuangalia zile kasoro na kwa kuwa Wizara na taasisi hizo zilishakutana na Kamati ya Sheria Ndogo kuangalia yale yaliyojiri katika sheria hizo na maeneo ambayo yanatakiwa kuboreshwa na kufanyiwa marekebisho, ninaomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kazi hiyo itafanyika vizuri.

Mheshimiwa Spika, tumekubaliana sasa kazi hii itafanyika vizuri sana chini ya uangalizi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuzingatia mipango na mikakati aliyoiweka Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Tungependa huko mbele tutoke kwenye hii namba ya 547 angalau iendelee kupungua kwa kiasi kikubwa na ikiwezekana sheria hizi zisiwe na makosa makubwa ambayo yanaweza kuhesabiwa ni makosa ya kusababisha Sheria hizo Ndogo kutokutumika vizuri ama kwenda kinyume na sheria mama na Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya naomba kwa unyenyekevu mkubwa niungane mkono na ripoti ya Kamati na niunge mkono maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwa niaba ya Serikali niendeleo kusema tuko tayari, tutaendelea kutoa ushirikiano kwa Bunge lako Tukufu kupitia Kamati mbalimbali kupokea maagizo na kuyafanyia kazi na kurudi kutoa taarifa ndani ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru naunga mkono hoja, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Jenista Mhagama nakushukuru sana kwa mchango wako. Sasa narudi kwa Mheshimiwa Mwenyekiti Mheshimiwa Mtemi Chenge ili kuhitimisha hoja yako sasa. Karibu sana, Karibu sana Mheshimiwa Mwenyekiti. (*Makofi*)

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO: Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuhitimisha hoja hii iliyo mbele ya Bunge lako tukufu. Nimshukuru sana Makamu wa Mwenyekiti wa Kamati hii Mheshimiwa William Ngeleja kwa kuwasilisha kwa umahiri sana hoja ya Kamati, na sote tumemsikia ame-*articulate* vizuri sana yaliyomo kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliopata nafasi ya kuchangia kwa kusema humu Bungeni. Lakini na wawili kwa kuchangia kwa maandishi. Nisingependa kuwatambua kwa majina lakini Waheshimiwa Wabunge wanane wamechangia hoja hii kwa kusema na wengine wawili kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, kazi ambayo tunaifanya kupitia Kamati yako hii ni kazi ya Kibunge ambayo tunaita *Parliamentary Control na Oversight ya Delegated Legislation*. Kwa Mabunge ndani ya Jumuiya ya Madola huu ndio utaratibu, kwasababu shughuli za Serikali ambazo ndizo nyingi sana zinagusa maeneo mbalimbali; na sheria ambazo zinaletwa Bungeni ambazo zinaruhusu kupitia Bunge kukasimu madaraka ya Bunge kwenda kwenye mamlaka nyingine kwanza ni nyingi na Bunge halina ule muda wote wa kuweza kwenda katika Sheria yenyewe kwenye *detail*.

Mheshimiwa Spika, sasa kitu ambacho sisi tunaendelea kushauri, na mimi hasa ninaendelea kuliomba Bunge lako Tukufu; mwenendo au mienendo katika dunia

ya sasa hivi kwenye upande wa kukasimu madaraka ya Bunge kwenda kwenye vyombo vingine, wanaofanya wahakikishe kwamba mnakasimu yale masuala ya msingi, yale ya sera na miongozo yake yote yanakaa kwenye Sheria Mama. Mnapompatia yule mnaemkasimisha mipaka inakuwa inafahamika. Nachukua mfano wenzetu wa Kenya, wameanza hii *approach* ya kwao unaweza ukasema sio *perfect* lakini wameanza.

Mheshimiwa Spika, kwenye sheria, *bill* inapoletwa muswada wa sheria unapoletwa Bungeni, ile sehemu ya mwisho ile ambayo inakuwa na kukasimu Mamlaka ya Bunge kwa Chombo kingine wanakuwa na *part* ambayo inaelezea kile ambacho kinaweza kwenda kukasimwa na mipaka yake kwa lengo hilo hilo na misingi ambayo itaonekana kwenye zile sheria ndogo.

Mheshimiwa Spika, mimi najua hii ni volition kwa sababu hatuwezi kuwa static kwa tumesimama tu. Sheria hii imetutumikia vizuri sana kwa kipindi kirefu tangu miaka ya 70.

Mheshimiwa Spika, na hii hoja inayosemwa na Wabunge naielewa. AG amelieleza vizuri sana. Nikichukua kwa upande wa, niliwahi kusema hapa Bungeni, ukichukua kwa upande wa tulikotoa hii sheria; wenzetu wana utaratibu ambao unaitwa; unauona kidogo kwa mbali kwenye sheria yetu; ule wa kuanza *negative*, tunaitaga *Negative Resolution Procedure*. Kwamba sheria inaruhusu Sheria Ndogo inaanza kutumika, inakuja kuwasilishwa Bungeni na Bunge linaweza sasa kusema hapana au la katika hatua hiyo ya kuwasilisha. Imeshawasilishwa imeanza kutumika; na ndio utaratibu wetu huu ambao unaukuta katika kifungu cha 38 (2); maana Bunge linaweza likasitisha hizo kanuni. Hata hivyo kusitisha kwake hakurudi nyuma, kwa yale yaliyotokea yametokea, inasitishwa kwa kuangalia kwenda mbele.

Mheshimiwa Spika, lakini pia wana utaratibu ambao tunaita ni *Affirmative Resolution Procedure*. Kuna mambo ya msingi katika baadhi ya sheria, ambayo mamlaka ambayo

imekasimiwa kazi hiyo inapoanza zoezi la kutunga kanuni ile rasimu wanaileta Bungeni ili sasa muone kama imekaa vizuri.

Mheshimiwa Spika, haya yote unayaangalia katika hali halisi ya nchi yako na mazingira yenu. Maana hoja si kusitisha shughuli za Serikali, ni kuhakikisha kwamba tunawezesha lakini na ile *control* ya Bunge kupitia taratibu ambayo kila Bunge limejiwekea; lakini Mabunge mengi ni Kamati kama hii ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Spika, mimi naamini kama Bunge lako litaendelea kuwa makini kama lilivyo, tunahakikisha kabisa kwamba hatutoi ukasimishaji ulio *ambiguous* ambao ni *vague* ambao ni *too broad* tutafanikisha sana shughuli za *oversight* na *control* ya Bunge kwenye sheria hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nachukua ahadi za Serikali, kwasababu tusipoweza ku-*train* watu wetu katika suala hili itakuwa ni tatizo. Na shughuli za Serikali zinapanuka kwa haraka sana na zitaendelea kupanuka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa unataka uwe na timu katika halmshauri zetu maana ndiyo tunazalisha sheria nyingi sana zinazogusa maisha ya Watanzania ya kila siku huko, *by laws* ni nyingi sana; lakini *regulations, rules, orders*, yote haya misingi yake Katiba ya Jamhuri ya Muungano Sheria Mama iliyoruhusu kukasimu na sheria zingine za nchi yamesema. Sheria zinapaswa zisomane, zisikinazane kama alivyokuwa anasema Mheshimiwa Sakaya. Sheria haziruhusu kukizana lazima zisomane mkiona kunakinzana mnanyoosha.

Mheshimiwa Spika, sina muda wa kuchukuwa sana shughuli ya muda wako na Bunge lako Tukufu. Mimi niishukuru sana Serikali kwa hayo mazuri waliyosema, tumefanya kazi vizuri sana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista na timu yake. Amekuwa mtu wa karibu sana na Kamati hii, Mwanasheria Mkuu na timu yake pale ambapo wamehitajika. Lakini hasa Mawaziri walioguswa na sheria ndogo hizi, Watendaji wao tunawashukuru sana kwa ushirikiano wao; lakini kwangu hasa kwa timu ambayo

umenipatia kwa *term* zote mbili, *term* ya kwanza miaka miwili na nusu na sasa tunapoitimisha Wajumbe wa Kamati wamekuwa. Wajumbe wa msaada mkubwa sana nawashukuru sana wamenipa msaada sana, Makamu Mwenyekiti sina maneno zaidi ya kuwaambia nakutoa shukrani zangu za dhati kwao.

Mheshimiwa Spika, nashukuru maneno ya shukrani walionipa wao kupitia Kamati lakini na Waheshimiwa Wabunge waliyoyoyasema. Narudia kusema, mimi ndivyo nilivyo, sina choyo ya kile ninachokifahamu huwa napenda kuwamegea na wengine walio na uihari wa kujifunza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo katika kuhitimisha hoja hii nikushukuru san asana kwa busara ulioyoitumia kuifufua tena kamati hii tumefanya mengi lakini tunapo enda tutaendelea kushauri Mungu atubariki, aturejeshe tena tuje tuyafanye hayo yapo mengi tunaweza tukaporesha kwa faida ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya naomba kutoa hoja kwamba Maoni na Mapendekezo ya Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo Kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na nane na Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge sasa yakubaliwe nayapitishwe na azimio ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

MHE. WILLIAM M. NGELEJA: Mheshimiwa Spika, Naafiki.

SPIKA: Ahsante sana waheshimiwa Wabunge hoja imetolewa na imeungwa mkono kwa kiwango kikubwa, na katika hatua hii sasa tayari kura mlikwisha zipiga na matokeo ambayo ninayo kupitia Mfumo wa Bunge Mtandao yanaonesha kwamba Wabunge wote waliopiga kura wameafiki hoja zilizomo katika Kamati hii na kwa hiyo kwa kweli imepita bila kupingwa.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Maoni na Mapendekezo ya Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo Kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Nane na Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge Yalipitishwa na Bunge)

SPIKA: Nichukuwe nafasi hii kukupongeza sana Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Makamu mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati hii. Kama tulivyosema hapo awali, kwa kweli mmefanya kazi kubwa, kazi kubwa sana mmechambua *volumes* and *volumes* za hizi Sheria Ndogo, kanuni mbalimbali na kadhalika. Mmezitendea haki mmezisaidia taasisi mbalimbali lakini zaidi mmewasaidia wananchi wetu katika kuwa na utawala bora hasa huko wanakoishi, ni jambo ambalo ni jema sana na nimuhimu kwa maisha ya watu wetu ya kila siku.

Kamati hii ni muhimu sana, na wajumbe hawa wa Kamati hii ninawashukuru kipekee. Kwa kweli sijui ilitokeaje ikawa ni timu hiyo tuliyoipata si walalamishi hata kidogo. Wakati Kamati zingine zikitaka kusafiri kila kukicha hii kamati haijawahi kuomba safari, kabisa. Wao wakifika ni kazi kazi Dodoma, wanamaliza Dodoma, Bunge linalofuata hawana maneno wanapiga kazi kabisa kabisa mwanzo mwisho.

Kwa hiyo nawashukuruni sana na kwakweli kama walivyosema wakina Mlinga, timu nzima ile imefika mahali imekuwa ni wanasheria wazuri kwa maana hiyo. Mheshimiwa Chege tukushukuru kwa ualimu huo na kuwalea vizuri wanakamati wako. Mheshimiwa Jenista tunakushukuru sana kwa kushirikiana na kamati mara kwa mara, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu na Maofisa wako pia ahsante sana.

Basi hapa ndipo tunapohitimisha shughuli za Kamati yetu hii. Kama alivyosema Mheshimiwa Chenge basi tuombeane kheri turudi Novemba; na ninatumaini tutarudi kivingine na kutakuwa na maboresho mawili matatu manne matano na kazi itazidi kuwa nzuri zaidi.

Basi kufikia hapa Waheshimiwa Wabunge niwaambie tu kwamba tunaelekea mwisho, ni vizuri Wabunge mkaanza kurudi rudi, wale ambao hawapo, mkaanza kurudi rudi hivi kwa sababu tunaelekea mwisho. Na kwasababu tunaelekea mwisho nadhani tukapeleka mambo kisayansi hapa hata hiyo tarehe 19 isifike. Kwa hiyo tuanze kurudi rudi, huo ndio ujumbe wa Spika, tuanze kurudi rudi maana yake mambo yanakwenda; nafikiri mmenisoma.

Basi baada ya hayo tuahirishe shughuli zetu za Bunge hadi siku ya Jumatatu Saa Nane mchana.

(Saa 10.27 Jioni Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatatu, Tarehe 8 Juni, 2020 Saa Nane Mchana)